

**KLOPP ASHANGAA LIVER KUTOIFUNGA MANCHESTER UTD**
UKURASA 21


# Nipashe

Jumanne Desemba 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581529

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com


UKURASA WA 4

**CHADEMA** yawasilisha barua bungeni kupinga ubunge kina Mdee



UKURASA WA 8

**Chalamila** aionya TRA rushwa, uonevu wafanyabiashara



UKURASA WA 19

**Chopa** kutumika kufikisha vifaa vya uchaguzi Mashariki DRC



## DC AANIKA KWA RCC:

# Fedha zinavyopenyezwa wanafunzi 'wachafuane'

• **Yumo** mtuhumiwa 'aliyechafua' wilaya tatu, anaswa...*Endelea ukurasa 3*




Rais Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo ya Mshindi wa Pili kipengele cha Mzalishaji Bora wa Vinywaji Baridi, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Bonite Bottlers Ltd, Raman Anantha Narayanan, katika hafla ya msimu wa 17 wa Tuzo za Rais kwa Wazalishaji Bora iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 3

### MASHAHIDI WATOFAUTIANA WASHTAKIWA WAACHIWA




MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru vijana watatu baada ya mashahidi 12 wa upande wa mashtaka kutoa...

UKURASA WA 17

### ACT YAONYA MASHEHA KUVURUGA AMANI Z'BAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo Zanzibar kimesema kama masheha wataendelea kuwabagua wananchi katika kutoa barua za...



## Ajira 25,000 zaja tena kwa vijana

UKURASA 5




# Serikali yajibu vilio vikuu vinavyotawala

• **Dola**, umeme, sukari, mafuta... *Endelea ukurasa 2*



2. Kuadimika kwa Dola za Marekani

3. Huduma ya umeme wa kupangiwa ratiba






4. Uhaba wa sukari viwanda vya ndani

**MICHEZO** WACHEZAJI YANGA WAMPA KIBURI GAMONDI UK.24 **KATUNI** UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Msemaji wa Kampuni ya Tumbaku Alliance One, Wakili John Magoti, tuzo ya ushindi wa uzalishaji mkubwa katika sekta ya viwanda vya tumbaku, hafla hiyo iliandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini. **Habari kamili Uk. 4** **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajibu vilio vikuu vinavyotawala

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi mambo makubwa kwa sekta ya viwanda ikiwamo kutatua tatizo la kukatika kwa umeme, akibainisha kuwa mwezi Januari mwakani, kinu cha kwanza katika Bwawa la Uzalishaji Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) kitawashwa ili kuruhusu uzalishaji.

Pia amesema tatizo la uhaba wa Dola za Marekani linashughulikiwa ndani ya nchi, akibainisha kuwa kwa sasa, Tanzania iko vizuri ina uwezo wa kutoa Dola milioni mbili kwa mtu kwa siku wakati wengine hata Dola 500,000 wameshindwa.

Rais Samia aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya msimu wa 17 wa Tuzo za Rais kwa Wazalishaji Bora (PMAYA), ambazo Kiwanda cha Vinywaji Baridi cha Bonite Bottlers Ltd kilitangazwa mshindi wa pili kwa upande wa Mzalishaji Bora wa Vinywaji Baridi.

Mshindi wa jumla katika tuzo hizo ni Kampuni ya Bia Tanzania Breweries (TBL), ikifuatiwa na Kiwanda cha Sigara Tanzania (TTC) na TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd katika nafasi ya tatu.

Akijibu hoja ya changamoto kubwa tatu ambazo wenye viwanda waliziainisha ikiwamo tatizo la umeme ambalo walimweleza huchochea kuongezeka gharama za uzalishaji, Rais Samia alisema mwezi Januari mwakani, kinu cha kwanza kati ya tisa katika Bwawa la Nyerere kitawashwa na kufuatiwa na cha pili mwezi Aprili.

"Jumla ya vinu vyote vipo tisa, cha kwanza kitawashwa Januari, cha pili Aprili tutakuwa tumekiwasha. Vile viwili tukiwasha tutakuwa na umeme wa kutosha sana utakaoingia kwenye Gridi ya Taifa.

"Pamoja na jitihada nyingine za gesi na solar (umeme wa jua) na mambo mengine, ninadhani hadi mwakani malalamiko mengi yatakuwa yamepungua," aliahidi.

Kuhusu changamoto ya pili ya tozo za stempu za kielektroniki (ETS) zinazolalamikiwa na wenye viwanda kuwa juu, Rais Samia alisema serikali iko kwenye mazungumzo na kampuni inayozitengeneza na kuna dalili njema kwa kuwa wamekubali kushusha gharama zake.

Pia alisema wanafanya mazungumzo na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili watumie mfumo wa kielektroniki kwenye stempu hizo.

Akitolea ufafanuzi changamoto ya tatu ya uhaba wa Dola ambayo inakabili nchi nyingi duniani, Rais Samia alisema Tanzania iko vizuri kulinganisha na wengine na serikali inaendelea kupambana kuhakikisha haiendi chini kwenye tatizo hilo kama wengine.

"Pamoja na changamoto tulizonazo, Tanzania tupo vizuri na tumewaacha wengine mbali kwenye ukanda wetu. Angalau sisi tunamudu kama alivyosema Waziri (wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji), angalau tumeongeza kiwango cha kutoa kwa siku.

"Kulivyokuwa na uhaba mkali, tulikuwa tunatoa Dola 500,000 kwa mtu kwa siku tukapandisha hadi milioni moja, tukapandisha tena hadi milioni mbili. Tuna majirani zetu leo hata Dola 500,000 kwa mtu kwa siku hakuna, hawana kwa hivyo tupo vizuri," alisema.

Kuhusu suluhisho la hilo, Rais Samia alisema wanaweza kulipata humu ndani ya nchi na kuainisha hatua za serikali zilizochukua zikiwamo za kupunguza kwa kiasi kikubwa yale mambo yanayoagizia nje.

"Mpango wetu ni kuangalia njia zote za kupunguza gharama za uagizaji ili tupunguze matumizi ya Dola. Tumeanza kujihusisha na mambo yanayoleta Dola harakaharaka na ndiyo maana mnasikia tunajihusisha sana na sekta ya kilimo," alisema.

Pia aliwaambia kuwa sekta ya utalii imekua na inasaidia kuleta Dola ndani ya nchi na kuieleza CTI na wenye viwanda kuwa watasaidia kupunguza uhaba wa Dola watakapozalisha na kuuza nje zaidi.

Kadhalika, Mkuu wa Nchi alisema katika kurahisisha biashara nchini, serikali imefungua milango ya uwekezaji bandarini huku akisisitiza kuwa hawawezi kuliepuka na kuikaribisha sekta binafsi kuungana na serikali, ili bidhaa ziende nje na kuingia nchini.

**SUKARI, MAFUTA**

Rais Samia pia alibainisha kuwa mwakani watafuta alichokiita "lugha ya Tanzania Tanzania" na kuanza kusafirisha sukari nje.

Vilevile, alisema suala la mafuta mwaka huu yamezalishwa mengi na kuondoa malalamiko, hivyo miaka miwili ijayo mahitaji ndani ya nchi yatatosheleza vya kutosha.

Aliwataka wenye viwanda kuwekeza zaidi hususan katika uongezaji thamani malighafi zilizomo nchini hasa bidhaa zinazotoka kiwanda kimoja kwenda kingine na serikali iko tayari kushirikiana nao.

"Maboresho na mazingira ya kufanya biashara ni safari, tunaendelea nayo. Ninadhani sasa hivi hakuna ambaye kodi imekuja kuchukuliwa kwa defender (gari la polisi), hakuna si ndio," alisema.

Jambo lingine alilolizungumzia ni Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, akiwaomba wenye viwanda washiriki kutoa maoni yao ili matarajio yao yawapo kwenye dira wanayopanga ya 2025-2050.

Pia aliwaomba wasaidie suala la ulipaji kodi na kufuata sheria za nchi kwa kuwa serikali imejitahidi kujenga mazingira mazuri kwa kuzifanyia kazi changamoto zinazoainishwa, pia uwazi katika utoaji wa fedha za uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) ili zisaidie kujenga madarasa na kuboresha elimu.

"Ahadi yangu kwenu, kwanza nimtake waziri wangu (Kijaji) awe karibu zaidi na wazalishaji wa viwanda, changamoto ni nyingi, zinapotokea zisichukue muda kutatuliwa.

"Ahadi yangu kwa wenye viwanda, serikali inafungua nchi zaidi na katika hili wengi wa nje wanataka kuja ndani. Ni furaha yetu, ninyi wa ndani mpokea wale wa nje ama mfanye kwa ushirika au mfanye kwa kuwahudumia wanaotoka nje.

"Tanzania ni jina kubwa, limekua ulimwenguni kiasi ambacho kila mtu anataka kuja Tanzania. Tanzania baada ya marekebisho ya mazingira ya kufanya biashara tupo kwenye sifa vizuri.

"Na sasa kuna kinyang'anyiro cha Afrika hasa kuhusu rasilimali, njia za kuchukua rasilimali zetu ni kuingia kwenye uwekezaji, nasi tuwabane kwa kuzalisha hapa ndani na si kuzichukua (kama malighafi)," alisema.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, alisema sekta ya viwanda inachangia takribani asilimia nane kwa mwaka katika Pato la Taifa, imeajiri asilimia tano ya waajiriwa wote nchini, yaani katika kila waajiri 100, watano wako sekta binafsi.

Pia alisema ni mwajiri wa tatu mkubwa baada ya sekta ya biashara na zaidi ya asilimia 20 ya makusanyo yote VAT inatoka huko na huchangia asilimia 18 ya fedha za kigeni.

Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alitaja vigezo vya kupata washindi hao kuwa ni pamoja na ufanisi katika uzalishaji, mauzo ya nje, uwekezaji katika teknolojia, uwiano wa kijinsia na mchango wao katika jamii.

Kuhusu changamoto ya maafa ya mafuriko na maporomoko ya tope, mawe na magogo katika mji mdogo wa Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara, Tenga aliyewahi kuwa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), alisema tayari CTI imewaelekeza wanachama wake kushiriki katika kutoa misaada.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu, alisema katika kuhakikisha taifa linanufaika na utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika, tayari wameandaa mkakati wa kitaifa wa utekelezaji mkataba huo ambao umeshakamilika na unatarajiwa kuzinduliwa Januari mwakani sambamba na kamati ya kitaifa ya kusimamia utekelezaji wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema huo ni mwaka wa pili mfululizo kuwa wadhamini wa tuzo hizo na kuwahakikishia kuwa wako tayari kutoa mikopo inayohitajika katika kuongeza uzalishaji.




Baadhi ya wajasiriamali wa mji wa Kiwira wilayani Rungwe, mkoani Mbeya wakiendelea na biashara ya ndizi katika hifadhi ya barabara kuu ya Mbeya -Kasumulu mwishoni mwa wiki, chini ya bango linalozuia kufanyika kwa biashara eneo hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mashahidi watofautiana kortini, hakimu aachia huru washtakiwa wote

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru vijana watatu baada ya mashahidi 12 wa upande wa mashtaka kutoa ushahidi unaotofautiana, hali iliyosababisha washindwe kuthibitsha kwamba Desemba 29, 2021 washtakiwa walisafirisha mirungi yenye uzito wa kilo 164.39 kwa kutumia usafiri wa bodaboda.

Vijana hao ambao walikuwa wakitetewa na Wakili Constantine Kakula ni Ahmed Ally, Mohamed Mbegu (35) na Ramadhani Mkude (42), wote wakazi wa Kitunda.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mkuu Ushindi Swalo wa mahakama hiyo, alisema upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi 12, ambao walitoa ushahidi wao kwa ajili ya kuthibitisha mashtaka dhidi ya vijana hao.

Hata hivyo, Hakimu Swalo alisema ushahidi uliotolewa na mashahidi wa upande wa mashtaka ulikuwa unatofautiana wakati wakitoa ushahidi wao dhidi ya washtakiwa.

Alisema askari waliokamata vielelezo hivyo waliieleza mahakama kuwa mirungi hiyo ilikuwa katika mifuko ya kaki, lakini mashahidi huru walioshuhudia ufungwaji wa vielelezo hivyo, walidai kuwa walikuta mirungi ikiwa wazi.

Pia maelezo ya onyo nayo yalikuwa yanatofautiana, washtakiwa walidai walifikishwa Kituo Kikuu cha Polisi Desemba 28, 2021 jioni, lakini askari waliokuja kutoa ushahidi wao walidai washtakiwa hao walipofikishwa polisi, walipelekwa Kitengo cha Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya (ADU) kwa ajili ya kuchukuliwa maelezo.

"Kwa maelezo haya, mahakama inaona kuwa yanaleta shaka na baadhi ya mashahidi wanatofautiana katika ushahidi wao," alisema.

Hakimu Swalo alisema kutokana na sababu hizo, mahakama hiyo inawaachia huru washtakiwa hao kutokana na Jamhuri kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Happy Mwakanyamale alidai kuwa kesi hiyo ilikuja kwa ajili ya hukumu na walikuwa tayari.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao ambao walikuwa wanadaiwa Desemba 29, 2021 katika eneo la Nyeburu lililoko Chanika, Dar es Salaam, majira ya usiku, walikutwa wanasafirisha mirungi yenye uzito wa kilo 164.39 kwa kutumia usafiri wa bodaboda.

Askari Polisi waliokuwa doria eneo hilo, walipewa taarifa za kuwapo watu wanauza mirungi eneo la Nyeburu na hivyo kufanya uchunguzi na kuwakamata watu hao.

DC AANIKA KWA RCC:

# Fedha zinavyopenyezwa wanafunzi 'wachafuane'

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VITENDO vya ukatili dhidi ya watoto vinaendelea kuripotiwa, safari hii Mkuu wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Suleiman Mwenda, amebaini fedha zinatumika kuchochea ukatili wa kingono katika baadhi ya shule wilayani mwake.

Katika hilo, Mkuu wa Wilaya Mwenda, bila kuainisha shule zinazohusika, amesema baadhi ya wanafunzi wanawaingilia kinyume cha maumbile wenzao wa kiume, wakiwapa fedha ambazo haijafahamika anayewafadhili kwa kuwa watoto hao wanatoka familia maskini.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki katika kikao cha Kamati ya Ushauri wa Mkoa (RCC) ambacho pamoja na mambo mengine, kilijadili mikakati ya kuboresha elimu kufuatia Mkoa wa Singida kutofanya vizuri kwenye Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, kidato cha pili na cha nne.

Mwenda alibainisha katika wilaya yake mambo kadhaa yanayosababisha wanafunzi kuishia njiani kutohitimu elimu ya msingi na sekondari ni pamoja na utoro, mimba, matukio ya ulawiti na baadhi kuolewa.

Alisema matukio ya ulawiti ni miongoni mwa yanayozorotesha elimu wilayani humo ambayo yamekuwa yakifanywa na wanafunzi wa shule za msingi ambao katika hali ya kushangaza, hufanya vitendo hivyo wakiwa na fedha za kuwahonga wenzao.

"Tuna hisia hawa watoto wanaofanya hivi vitendo kuna watu wako nyuma yao, kwa sababu wana fedha za kuwahonga wenzao japo wazazi ni maskini, wapo wengine wanatembea na mafuta maalum ya kufanya shughuli hiyo, tunajiuliza hivi vitu wanatoa wapi?" Alihoji.

Mwenda alisema katika tukio mojawapo, kijana mmoja kutoka Kata ya Ndulumi, alikamatwa wilayani Iramba kwa kujihusisha na vitendo vya ulawiti.

"Lakini (kijana huyo) alipopewa dhamana akatoroshwa, alikwenda Manyoni, nako akakamatwa, alipopewa dhamana akatoroka na kwenda mjini Singida, nako akafanya vitendo vya kulawiti akakamatwa tena," alisema Mwenda.

Hayo yanajiri kipindi ambacho mwanzoni mwa mwaka huu, gazeti hili liliripoti baadhi ya shule mkoani Kilimanjaro, walimu wake kuwafundisha watoto kufanyiana mchezo huo mchafu.

Baada ya kuchapishwa ripoti hiyo, serikali kupitia Wizara ya Elimu, iliunda timu ya uchunguzi ambayo licha ya kuongozwa na Kamishna wa Elimu, ilizuiwa kuingia katika baadhi ya shule kufanya uchunguzi.

Mwenda alisema matukio mengine yanayofifisha maendeleo ya elimu ni baadhi ya wasichana kutoka Iramba kupelekwa jijini Dar es Salaam kwa ahadi ya kwenda kufanya kazi za ndani, lakini wakifika huko baadhi yao hutumikishwa kwenye madanguro na katika baa.

Alisema matukio hayo aliyoyataja ni machache, yamekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya elimu na kushauri umuhimu wa kufanya kazi ya ziada kukabiliana na vitendo hivyo ili kuinua kiwango cha elimu mkoani Singida.

**WANAFUNZI WAOZESHWA**

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya Mwenda alisema katika Shule ya Msingi Mwamapuri iliyoko wilayani Iramba, imeingia katika rekodi mpya baada ya wanafunzi wanane kuolewa wakiwa wanaendelea na masomo.

"Katika Shule ya Msingi Mwamapuri mwaka jana (2022) ilikuwa ya mwisho kimkoa ambayo kati ya wanafunzi 23 waliofanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, wawili tu ndio waliofaulu na baada ya kufanya uchunguzi tulibaini shule hii ina changamoto ya wanafunzi kuolewa kabla ya kuhitimu.

"Nilikwenda (mwezi) Februari kwa kutuma timu yangu kuchunguza, wakakuta watoto wanane wameshaolewa wakiwa bado wako shuleni wakawa wanaambiwa, 'waume zenu wanawasubiri mmalize ili mkakabidhiwe'," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliiagiza idara ya elimu kuhakikisha shule 12 zilizojengwa kupitia mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya shule za msingi (Boost) zinasajiliwa na apewe ripoti Ijumaa ya juma hili.

The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Arusha and Zanzibar**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 28th December, 2023.**

# CHADEMA yawasilisha barua kwa Spika kupinga ubunge kina Mdee

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimewasilisha barua katika Ofisi ya Spika wa Bunge kukumbushia kuondolewa bungeni wabunge 19 ambao chama hicho kilishawafutia uanachama.

Pia kimewasilisha barua hiyo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Ofisi ya Rais.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kati, Emmanuel Masonga, alibainisha hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kutekeleza agizo la Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika la kuwasilisha barua za kukumbushia uamuzi wa Kamati Kuu ya chama hicho kwa Ofisi ya Spika wa Bunge.

"Leo (jana) nimetekeleza maagizo ambayo nilipewa jana (juzi) na Katibu Mkuu kwa maandishi kwamba niliwasilishe barua ambazo ameandika yeye kwa Spika, lakini pia Ofisi ya NEC, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa pamoja na Ofisi ya Rais.

"Leo (jana) tangu saa moja asubuhi nimeanza utekelezaji maagizo hayo na tayari Ofisi ya Spika wa Bunge imepokea na kutia saini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa wamepokea na kutia saini, NEC wamepokea na kutia saini na Ofisi ya Rais wamepokea na kutia saini kupokea barua hiyo," alisema.

Kiongozi huyo lisema barua hiyo ya Katibu Mkuu wa CHADEMA inakumbushia uamuzi wa Kamati Kuu ya chama hicho kuwafukuza uanachama wabunge 19 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na chama chao kama mdhamini kilishawaondolea sifa ya kuwa wanachama.

"Hivyo, Katibu Mkuu anaikumbushia Ofisi ya Spika wa Bunge pamoja na ofisi zingine kutekeleza maagizo yalitolewa na Kamati Kuu ya chama kutekeleza ombi la kuwaondoa bungeni wabunge hao 19, maeneo yote ambayo Katibu Mkuu aliniagiza kufikisha barua hizo nimefikisha," alisema Masonga.

Kadhalika, alisema chama kinawataka wanachama hasa wa Kanda ya Kati kuendelea kuwa watulivu wakati wanajadiliana na wanasheria kuhusu sakata hilo.

"Wanachama wanapaswa kuendelea na shughuli za kuimarisha chama kwa kuandikisha wanachama wapya na kufanya uchaguzi wa ndani ya chama na kujiandaa kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, ili kujipanga na Uchaguzi Mkuu kupata wabunge na kuongoza nchi," alisema Masonga.

Hatua hiyo ya CHADEMA imechukuliwa siku chache baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutoa uamuzi kuhusu shauri lililofunguliwa na wabunge hao, wakiongozwa na Halima Mdee, Mbunge wa zamani wa Kawe.



Ofisa Ardhi mteule Wilaya ya Muheza, Tanga, Selestin Liweje (kushoto), akizungumza na wananchi wa Kata ya Majengo juzi kuhusu waliopimiwa viwanja kwenda kuchukua hati zao Ofisi ya Msajili wa Hati mkoani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wadau waitwa kutoa maoni muswada Sheria ya Uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI mbili za Bunge zinawaalika wadau kutoa maoni kuhusu miswada mitano ya sheria iliyosomwa kwa mara ya kwanza Novemba 10, mwaka huu wakati wa Mkutano wa 13 wa Bunge.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa Ofisi ya Bunge, Dodoma, miswada hiyo ni ya: Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023; Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023; Muswada Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023; na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mkutano wa kupokea maoni ya wadau wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria utafanyika Januari 6 na 8, mwakani jijini Dodoma.

Vilevile, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji wa Umma (PIC) inawaalika wadau kutoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023, kikao kitafanyika Januari 10, mwakani katika Ofisi ya Bunge.

"Kamati zinawaalika watu wote wenye maoni kuhusu miswada hiyo kufika na kuwasilisha maoni yao kabla haijapelekwa katika hatua nyingine. Pia wanaweza kutuma kwa njia ya posta, anwani ya Bunge, barua pepe na tovuti na kwamba watakaofika watatakiwa kuthibitisha ushiriki wao,"alisema.

**Taarifa hiyo ilieleza kuwa mkutano wa kupokea maoni ya wadau wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria utafanyika Januari 6 na 8, mwakani jijini Dodoma.**

# Alliance One yang'ara tuzo za Rais za Wazalishaji Bora

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Alliance One Tobacco Tanzania Limited (AOTTL) yenye makao makuu yake Morogoro, imetwaa tuzo kubwa ya viwanda vya kusindika tumbaku katika msimu wa 17 wa Tuzo za Rais kwa Wazalishaji Bora (PMAYA) zilizoandaliwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), ikiwapiku wazalishaji wengine wengi katika kipengele hicho.

Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi katika tuzo hizo zinazofanyika kila mwaka, akikabidhi zawadi kwa washindi jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Msemaji wa kampuni hiyo, Wakili John Magoti alipokea tuzo kwa niaba ya kampuni.

Akitoa maelezo kuhusu kampuni pembeni mwa PMAYA, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Ephraim Mapoore, alisema Alliance One imeshinda tuzo hiyo si kwa bahati mbaya au bila kutarajiwa, bali ufanisi mkubwa wa kampuni hiyo katika kilimo bora na ufuasi wa taratibu za mikataba na wakulima iliyoingia nao kandarasi.

Kampuni ya Alliance One Tobacco Tanzania (AOTTL) imelipa jumla ya Dola za Marekani milioni 71.9 (Sh. bilioni 179.8) kwa wakulima zaidi ya 12,000 walioingia mkataba nayo wa tumbaku nchini msimu huu. Ni malipo yaliyolipwa kwa wakati, yaliyotokana na tumbaku yenye ubora wa juu.

Vilevile, kampuni imelipa Dola milioni 1.81 (Sh. bilioni 4.6) kwa ada za Vyama vya Ushirika vya Masoko ya Kilimo (AMCOS) kwa mwaka huu.

Kampuni pia imelipa Dola 780,000 (Sh. bilioni 1.95) kama ushuru kwa vyama vya ushirika vya tumbaku, ambavyo ni vyombo vikuu vya ushirika vilivyoanzishwa.

Pia imelipa jumla ya Dola za Marekani milioni 1.72 (Sh. bilioni 4.3) kama malipo ya mazao, kiasi ambacho kwa kawaida hulipwa moja kwa moja kwa wilaya mbalimbali inazofanyia kazi.

Malipo haya yalifanywa kwa kuzingatia agizo la serikali la hivi karibuni kwamba malipo yote ya tumbaku kwa wakulima yanapaswa kufanywa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kukamilika kwa mnada wa soko na malipo yote lazima yafanywe kwa Dola ya Marekani.

Kwa kawaida kampuni hutenga Sh. milioni 400, kila mwaka kwa ajili ya kurudisha sehemu ya faida kwa jamii inayozunguka maeneo ya shughuli zake, ikichangia katika miradi ya maji, afya na elimu.

Mwaka huu kampuni imetoa vifaa vya shule vyenye thamani ya Sh. milioni 222.762 kwa shule mbili za msingi za Morogoro ambazo ni Kingolwira na Bungo. Msaada huo uliowanufaisha moja kwa moja jumla ya wanafunzi 3600 katika shule zote mbili, ulitumika katika ujenzi wa madarasa na vyoo.

Ni kwa mwaka huu pia kampuni hiyo imetoa kompyuta tatu za kisasa na vifaa vingine vya kisasa vyenye thamani ya milioni 8.8 kwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kusaidia kufanya upasuaji wa mifupa.

Kadhalika, kampuni imetoa msaada wa kompyuta kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya kupambana na uhalifu.

Kampuni hiyo pia imetekeleza miradi ya upandaji miti katika wilaya tatu za Mkoa wa Kigoma, jumla ya ekari 1412.5 zimepandwa na kusimamiwa tangu mwaka 2014.

Kampuni hiyo ilipanda miti kwa kushirikiana na wakulima walioingia nao ubia katika wilaya tatu za mkoa huo ambazo ni Uvinza, Buhigwe na Kasulu.

Kampuni hiyo pia mwaka huu imezindua eneo la Ngukumo wilayani Nzega kwa ajili ya usambazaji wa kuni endelevu kwa wakulima wake wa tumbaku walioingia mkataba wenye jumla ya hekta zaidi ya 7,000 chini ya usimamizi wa pamoja wa misitu.

Alliance One ilifungua kiwanda chake cha usindikaji mnamo 1998 na imekuwa inafanya kazi kwa mafanikio tangu wakati huo bila kukosa msimu wowote wa mazao na kwa sasa ina wafanyakazi 350 wa kudumu na wanaolipwa pensheni pamoja na wafanyakazi wa msimu 3,000 kila mwaka.

# Ajira 25,000 zaja tena kwa vijana serikalini

**Na Augusta Njoji,** SIMIYU

SERIKALI imesema mwezi ujao inatarajia kutangaza nafasi za kazi 25,000 kwenye sekta za afya na elimu ili kukabiliana na upungufu wa watumishi uliopo.

Katika ziara yake ya kukagua miradi na kuongea na watumishi mkoani Simiyu jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema kuwa baada ya kukamilisha taratibu za serikali, mkoa huo utaongezwa watumishi walioombwa kwenye kada mbalimbali zikiwamo afya na elimu.

Alisema wapo watanzania wanahitaji kufanya kazi, hivyo walipopo kwenye ajira wanapaswa kuwajibika ipasavyo kutoa huduma kwa wananchi.

"Ukishikwa shikilia, ukipata nafasi ishikilie kama hamwamini angalieni tuliokuwa nao serikalini huko, nje hali zao zikoje, mkiweka kipimo hicho mtajiongeza kuwa kuna uhitaji wa kuwahudumia watanzania wenye nchi yao, asije pale ukamfokea ukashindwa kumhudumia," alionya.

Waziri huyo alisema katika kanzidata ya TAMISEMI mna watu wanaoomba kazi kwenye sekta ya afya 100,000 na kwenye elimu ni hivyohivyo.

Aliwaomba watumishi kufanya kazi kama zao na wasiwe tayari kuona serikali ikiharibikiwa kwa uzembe wao.

"Fanyeni kazi kama ya kwenu, kama mtaji dukani kwako, huu ni mtaji ukianguka hata wewe huna chako, nendeni mkajishushe kwa wananchi, muwe wakarimu kwa wananchi haikupunguzii chochote, hata kama ni Mkuu wa Wilaya, cheo chako kipo palepale. Ukijipandisha mabega kuporomoka kwake ni hatari," alisema.

Alionya kuwa serikali haitafumbia macho watumishi wa afya watakaosababisha vifo vya wajawazito na watoto.

"Ninawapongeza Simiyu kwa kuwa mkoa wa kwanza kupunguza vifo vya wajawazito na watoto, tumekwenda Kagera tukaambiwa hospitali inajulikana ni chinjachinja, hawatoi huduma bora, tusikie mjamzito hajahudumiwa kwa sababu hana vifaa kama ilivyotokea kule Mara mama amefariki dunia na vichanga vyake pacha wakati vifaa vipo...," alionya.

Alitolea mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema amekuta Kituo cha Afya Kanyerere kimekamilika na kina vifaa, lakini kimekaa mwaka mzima bila kutoa huduma kwa wananchi huku viongozi wa halmashauri wakiwa hawana majibu ya sababu zinazosababisha kisitoe huduma wakati wananchi wanaendelea kutembea umbali wa kilometa 16 kufuata huduma za afya.

Kuhusu ujenzi wa shule za mradi wa uboreshaji elimu ya awali na msingi (BOOST) na wa elimu ya sekondari (SEQUIP), Mchengerwa alisisitiza kuwa na kikao na Wakuu wa Mikoa Desemba 30, mwaka huu na kueleza pia walivyojipanga kupokea wanafunzi mwezi Januari 2024, uandikishaji wanafunzi, ushirikishaji wazazi na walezi.

"Tunatarajia kuwa na Mheshimiwa Rais tumemwomba ili awasikie na ajue mkurugenzi gani hawajibiki, utaratibu huu utatuweka karibu sana maana hapo kati tulijisahau sana tukasahau majukumu yetu, tukasahau wananchi," alisema.

Kadhalika, alisema wakurugenzi wa halmashauri moja ya kigezo watakachopimwa kwenye utendaji kazi wao ni namna wanavyotengeneza vyanzo vipya vya mapato na upangaji wa bajeti za miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Nimemwambia Katibu Mkuu awaandikie tunataka kila mwaka mkurugenzi atengeneze vyanzo vipya viwili vya mapato kwa sababu haiwezekani muwe na vyanzo vilevile vya mwaka 2000, hamjiongezi," alihadharisha.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, alisema mkoa huo una uhitaji wa watumishi 21,000 na waliopo ni 12,000, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 9,000 na kuiomba serikali kuondoa upungufu huo hasa kwa kada za afya na elimu.

**VIGOGO WACHUNGUZWA**

Katika hatua nyingine, Waziri Mchengerwa amesema ofisi yake imetuma timu ya wataalamu kuchunguza maeneo ambayo wakurugenzi na viongozi wa serikali waliingilia majukumu ya wakuu wa shule kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu nchini.

Alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wake na Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA) uliofanyika jijini Mwanza.

Alisema wapo wakuu wa shule miongoni mwao wameshindwa kumaliza baadhi ya shule hizo kutokana na kuingiliwa majukumu na wakurugenzi na viongozi wakubwa wa serikali.

Wapo Wakurugenzi ambao walikuwa wanawaingilia kwenye "meneo yenu, wapo wakurugenzi wa halmashauri tuliwakabidhi nyenzo na fedha za kufanya kazi ninyi walimu kusimamia baadhi ya miradi, lakini baadhi ya watendaji wa serikali wengine viongozi wakubwa kwenye serikali wamewaingilia.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI NA 22 YA 2022**
**BITALIHO RUHERE ...........................MDAI**
**DHIDI YA**

1 LAZARO CHIBAGO LECHIPYA
2 DAVID C. MAZIKU
3 THE REGISTERED TRUSTEES OF AFRICA BENEDICTINE SISTERS OF ST. AGNES CHIPOLE
4 THE REGISTERED TRUSTEES OF CHRIST TO ALL PEOPLE CHURCH
5 YUSUPH H. ABUU
6 DICKSON EVALIST
7 NICKSON JACKSON
8 DEODAS PIUS
9 EMMANUEL JACKSON
10 MOSES REBEN
11 FREDY OSWADY
12 MATHAYO BWELI ......WADAIWA
13 ARON EXAUDY
14 EMANUEL
15 PATRICE WAMILY KUGULULYE
16 JAMES RAPHAELY KALALU
17 IMAN ONESMO MAHELELA
18 MAGOMBA
19 PLOTUS
20 NEEMA JEREMIA
21 OMARY

KWA:
1 LAZARO CHIBAGO LECHIPYA
2 DAVID C. MAZIKU
3 THE REGISTERED TRUSTEES OF AFRICA BENEDICTINE SISTERS OF ST.AGNES CHIPOLE
4 THE REGISTERED TRUSTEES OF CHRIST TO ALL PEOPLE CHURCH
5 YUSUPH H. ABUU
6 DICKSON EVALIST
7 NICKSON JACKSON MDOL
8 DEODAS PIUS
9 EMMANUEL JACKSON
10 MOSES RUBEN
11 FREDY OSWADY
12 MATHAYO BWELI
13 ARON EXAUDY
14 EMANUEL
15 PATRICE WAMILY KUGULULYE
16 JAMES RAPHAELY KALALU
17 IMAN ONESMO MAHELELA
18 MAGOMBA
19 PLOTUS
20 NEEMA JEREMIA
21 OMARY

**POPOTE PALE WALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 22 YA 2022**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. A.J. MAMBI, JAJI** wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 15/2/2024.
**HIVYO;** Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** Hamtafika nyinyi au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo nyinyi au wakili wenu kuwepo.
**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 19/10/2023

.............................................................
**NAIBU MSAJILI**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF INFORMATION, COMMUNICATION AND INFORMATION TECHNOLOGY**

## APPOINTMENT TO POSITION OF A MEMBER OF BOARD OF DIRECTORS OF THE TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY (TCRA)

**1. Background**
The Chairman of the Nomination Committee, established under section 8 (1) of the Tanzania Communications Regulatory Authority Act. No. 12 of 2003, invites Tanzanians with relevant qualifications as spelt out herein to apply for appointment to fill vacant position(s) available in the TCRA Board. Attention is hereby drawn that all applicants are required to observe the provision of section 7 (5) and section 11 of the TCRA Act No. 12 of 2003 as well as the TCRA Code of conduct relating to conflict of interest.

**2. Qualifications required:**
As per the First Schedule of the TCRA Act 2003, the following are the minimum qualifications for appointment to the TCRA Board:

1. Should be a graduate of a recognized University;
2. Must have at least 10 years experience in one or more of the fields of Management, Law, Economics, Finance, Engineering, Broadcasting, ICT or related fields;
3. Have knowledge of the Communication Industry;
4. Should satisfy the Nomination Committee that he/she is unlikely to have a conflict of interest under Section 11 of the Communication Regulatory Authority Act, No.12 of 2003;
5. Be willing to serve as Member to the Board.

**3. Mode of Application**
a) All interested qualified candidates should submit their letter of application along with a detailed curriculum Vitae (CV). The CV should include names, email address, telephone, current work position as well as email and mobile No. of three (3) referees with at least one being the current or last employer. All applications should be addressed to:

**The Chairman,**
**Nomination Committee,**
**Ministry of Information, Communication and Information Technology,**
**Mtumba Goverment City,**
**P.O. Box 677,**
**40470 DODOMA**

b) The envelope should be marked on top: 'The Chairman of Nomination Commitee'.
c) The applications to be submitted physically or Postal Address or Email Address: **nominationcommittee@mawasiliano.go.tz.**
4. Women with the requisite qualifications are encouraged to apply.

**5. Deadline for Submission**
Applications should reach to the Chairman of Nomination Commitee within fourteen (14) days from **18th December, 2023** as the date of first appearance of this publication to **07th January, 2024 before 15:30hrs EAT.**

177625

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Marufuku ya RC utupaji taka ovyo itekelezwe

**JIJI** la Dodoma hivi sasa ni maarufu kutokana na kuwa makao makuu ya Tanzania na shughuli nyingi za kiserikali kuhamia huko.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vikao vyake vinafanyikia huko baada ya kutoka Karimjee, jijini Dar es Salaam, wakati huo likiwa la chama kimoja.

Umaarufu wa jiji hilo unatokana na ndoto za Rais wa Kwanza, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ya kutaka Dodoma kuwa makao makuu ya Tanzania.

Ukiangalia kwenye Ramani ya Tanzania, Dodoma iko katikati kwa hiyo ni rahisi kwa wakazi wa mikoa mingine kufika.

Kutokana na umaarufu wake, haitapendeza mji huo kuwa katika hali ya uchafu kwasababu wageni wengi wanautembelea na vilevile, baadhi ya ofisi za mabalozi wa nje ya nchi wana ofisi zao huko.

Katika kuhakikisha mkoa huo unakuwa katika hali ya usafi Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, amepiga marufuku abiria wanaotumia mabasi kutupa taka ovyo pembezoni mwa barabara na kuonya watakaobainika watakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Akionesha mfano wa kuweka mkoa huo katika hali ya usafi, ameshiriki na wananchi wa Kata ya Mnadani na Miyuji kusafisha mazingira akihusisha taasisi mbalimbali zinazojihusisha masuala ya usafi wa mazingira.

Mkuu wa Mkoa amekumbusha kuwa wageni mbalimbali wanaoingia kutoka mikoa mbalimbali wanatarajia wanapofika makao makuu wakute unafanana na hadhi ya jina lake.

Madereva na makondakta wanaofanya kazi katika magari hayo wanawajibu wa kuwaelimisha abiria wao kuzingatia usafi wa mazingira na umuhimu wa kuweka vyombo maalum vya kuhifadhia taka ili abiria wao wasichafue mazingira.

Kuna abiria ambao wanapenda kula kula wanapokuwa wanasafiri na wao huwa wachafuzi wakubwa wa mazingira kwa kutupa mabaki ya chakula na vifungashio vyake na tena wanatupa barabarani bila aibu.

Mkuu wa Mkoa anapotoa agizo izingatiwe kuwa ni amri na lazima wasaidizi wake wahakikishe wanalisimamia ili utekelezaji ufanyike.

Wakazi wa mkoa pia wanawajibu wa kujenga utamaduni wa kupenda kufanya usafi bila kulazimishwa ili kuepuka kutozwa faini.

Hili la wananchi kutakiwa kuwa na utamaduni wa kupenda usafi ni la muhimu, kwa sababu usafi huanzia nyumbani mtu anakoishi.

Watu ambao wanaonekana wakichafua mazingira ovyo, hao mpaka nyumbani kwao ni wachafuzi. Anayependa usafi hawezi kufanya hivyo hata akiwa nje ya nyumbani kwake.

Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, ameahidi kuendelea kusimamia suala la usafi wa mazingira na kuwachukulia hatua kali za kisheria watakaokaidi.

Katika hili hakuna kuoneana aibu na sheria lazima ichukue mkondo wake kwa wanaochafua mazingira kupewa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Kila mwananchi katika eneo lake ni lazima afanye usafi na iwe tabia ya mtu kuanzia nyumbani kwake na liwe somo hata kwa watoto waliopo ndani ya familia bila kusubiri kusukumwa au kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kitu cha msingi ni kukumbuka kuwa agizo la Mkuu wa Mkoa ni lazima litekelezwe na lisifanywe kama nguvu ya soda, liwe endelevu ili wananchi wazoee usafi.

Kwanini mkoa wa Kilimanjaro umefanikiwa katika usafi? Ni kwasababu wananchi wenyewe wanakuwa askari wa mwenzake na adhabu hutolewa papo kwa papo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge


Sabato Kasika

# Kidato cha kwanza 2024, msisubiri kusakwa mitaani

**BAADA** ya matokeo ya mtihani wa darasa la saba wa mwaka huu kutangazwa, wanafunzi 1,092,984 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka ujao katika mchakato unaotangazwa hivi karibuni.

Aidha, wengine 1,410 wamepangwa katika baadhi ya shule za sekondari za mkondo wa amali za kihandisi, ikiwa ni kuanza utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, wakati akitangaza matokeo hayo jijini Mwanza juzi.

Katika ufafanuzi wake, kati ya idadi hiyo wasichana ni 585,051 na wavulana 507,933 wamefaulu na kupangiwa shule za sekondari za serikali ili waanze masomo ya kidato cha kwanza Januari, 2024.

Waziri huyo anafafanua kuwa idadi hiyo inajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum 3,587 wakiwamo wasichana 1,590 na wavulana 1,997 na kwamba wanafunzi waliopangiwa shule 48 za bweni za kitaifa ni 5,606 sawa na asilimia 0.5, katika shule teule za mikoa ni 17,412 sawa na asilimia 1.6 na shule 4,566 za kutwa ni 1,069,966 sawa na asilimia 97.9.

Baada ya maelezo hayo, ngoja nirejee katika hoja yangu ambayo unahusu utoro wa baadhi ya wanafunzi ambao umekuwapo kwa muda mrefu kila mwaka wa masomo unapoanza na kusababisha serikali kuanzisha msako.

Mwaka 2023 ndio huo unaelekea ukongoani ili mwaka wa masomo uanze Januari 2024 panapo majaliwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na darasa la kwanza katika shule mbalimbali.

**Mwaka 2023 ndio huo unaelekea ukongoani ili mwaka wa masomo uanze Januari 2024 panapo majaliwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na darasa la kwanza katika shule mbalimbali.**

Kwa kuwa kumekuwapo na utoro kila mwanzo wa mwaka kwa wanafunzi wa sekondari, ninadhani kuna haja ya kuanza mapema mikakati ya kukabiliana na utoro huo.

Waziri amekaririwa na vyombo vya habari akitoa wito kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, viongozi na watendaji wa halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu kuondoa utoro huo.

Anataka wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo yao mwezi Januari, 2024 bila vikwazo vya aina yoyote ili kutekeleza azma ya serikali ya utoaji wa elimu bila ada.

Anawaagiza wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kufanya maandalizi ikiwamo ujenzi wa miundombinu, kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao inakamilika kwa wakati.

Wakati waziri anatoa maelekezo hayo, ninadhani ipo haja, kujua chanzo cha utoro huo wa kila mwaka na kukitafutia ufumbuzi wa kudumu na kama hakijajulikana, inawezekanaa mwaka ujao utoro huo ukaendelea.

Imekuwa ni kawaida kusikia zaidi ya wanafunzi 200 waliochaguliwa kujiunga na shule fulani ya sekondari hawajaripoti, na kusababisha serikali kuanzisha msako wa nyumba kwa nyumba.

Utoro wa aina hiyo si rafiki kwa elimu, hivyo ingekuwa ni vyema kama wanafunzi wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza mwaka ujao wasisubiri kusakwa bali shule zikifunguliwa waende waanze masomo.

Wakati mwingine inawezekana wapo ambao wazazi wao huwahamishia katika shule nyingine badala ya zile walizochaguliwa, hilo ni jambo la kawaida, lakini sidhani kama wanafunzi 100 au 200 waliochaguliwa shule moja wazazi wao wanaweza kuwahamisha wote kwa mara moja.

Hapo ni wazi kutakuwa na jambo ambalo halijakaa sawa. Yaani wanafunzi wenyewe wanaweza kuwa ni watoro au wazazi wao kukataa kuwapeleka shule ili wafanye majukumu mengine ya nyumbani.

Ninaamini ufuatiliaji ukifanyika unaweza kubaini chanzo cha utoro huo wa kila mwaka, kwani inashangaza kuona mwanafunzi anasoma miaka saba shule ya msingi anafaulu kwenda sekondari, kisha anakuwa mtoro.

## Rais Samia aikabidhi NBC tuzo ya heshima ukuzaji sekta ya viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekabidhi tuzo ya heshima kwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kutambua mchango wa benki hiyo katika kufanikisha msimu wa 17 wa Tuzo za Rais za Wazalishaji Bora wa Viwanda (PMAYA).

Benki hiyo ambayo imekuwa mdhamini mkuu wa tuzo hizo za kila mwaka kwa mwaka wa pili mfululizo, pia imetunukiwa tuzo hiyo kwa kuchochea kasi ya ukuaji wa sekta ya viwanda nchini kupitia huduma zake za kifedha.

Rais Samia alikabidhi tuzo hiyo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo hizo iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Tuzo za PMAYA huandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), zikilenga kutambua mchango wa sekta ya viwanda kiuchumi na kuchochea ushindani wa utoaji huduma miongoni mwa viwanda hivyo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Rais Samia mbali na kuwapongeza wadhamini mbalimbali wa tuzo hizo ikiwamo NBC, pia aliangazia masuala mbalimbali yanayohusu mustakabali wa sekta ya viwanda nchini hususani upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika na kutambua mchango na umuhimu wa huduma za kifedha katika kukuza ustawi wa sekta ya viwanda na kuchochea ushindani katika soko la ndani na nje ya nchini.

Awali akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Sabi, alisema benki hiyo imejipanga katika utoaji huduma na fursa mbalimbali kwa wadau wa sekta ya viwanda nchini ikiwamo mikopo ya aina zote hususani ile inayolenga kuongeza uzalishaji viwandani.

Pia huduma za bima na kinga dhidi ya majanga na mabadiliko ya riba, huduma za malipo ya ndani na nje ya nchi ikiwamo ukusanyaji mapato ya serikali na utoaji wa mikopo inayowezesha biashara za kimataifa (International Trade Financing).

"Pamoja na huduma za kibenki kwa wadau wa viwanda, NBC kwa sasa tunatekeleza mkakati wetu wa kukuza huduma rasmi za kibenki kwa makundi maalum ikiwamo wafanyabiashara wadodo na wa kati (SME), wanawake na wajasiriamali," alisema Sabi.

Kwa mujibu wa Sabi, ushirikiano baina ya wadau wakubwa wa viwanda na makundi hayo maalum utachochea zaidi kasi ya ukuaji wa uchumi nchini kutokana na mwingiliano mkubwa baina yao.

Sabi ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Benki Tanzania (TBA), alitumia fursa hiyo kuwasilisha kwa Rais Samia utayari wa taasisi zote mwanachama wa umoja huo katika kutoa huduma kwa sekta ya viwanda nchini huku akipongeza jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuweka mazingira rafiki ya biashara ili kufungua nchi kiuchumi na kuvutia uwekezaji.

"Jitihada hizi za serikali zinazoonekana katika maeneo mengi ikiwamo utalii, miundombinu, mauzo ya bidhaa za nje, ukuaji wa sekta za madini na maeneo mengine mengi ni matunda ya juhudi hizo za serikali ambazo zimezaa fursa kubwa kwa taasisi za fedha nchini. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais," alipongeza Sabi.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, alionyesha kuguswa zaidi na ushirikiano uliopo baina ya wadau wa viwanda nchini pamoja na serikali kama ilivyo pia baina ya wadau hao na taasisi za fedha nchini huku kipekee akiipongeza Benki ya NBC kwa namna inavyoshirikiana na wadau hao kupitia huduma zake pamoja na udhamini wa benki hiyo kwenye matukio mbalimbali yanayoandaliwa na wadau hao ikiwamo Maonesho ya Kimataifa ya Viwanda (TIMEXPO) na tuzo za PMAYA.



Kiongozi wa Idara ya Wanawake Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis, Dar es Salaam, Egra Kerenge, akiendesha semina kwa mabinti wa kanisa hilo juzi, iliyohusu makuzi ya ujana, malezi ya kiroho, maisha ya usafi wa mwili na mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Serikali ihamishe watu wote wanaoishi maeneo hatarishi'

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

RAIS wa Chama cha Wachungaji na Maaskofu nchini (TPA), Askofu Dk. Musa Mlawi, ameshauri serikali kutumia wataalamu wake kuhamisha watu wote wanaoishi kwenye maeneo hatarishi ili kuondokana na maafa kama yaliyotokea wilayani Hanang, mkoani Manyara.

Ushauri huo unatolewa huku vifo vya watu vilivyosababishwa na maporomoko ya matope, mawe na magogo katika mji wa Kateshi wilayani Hanang vikiwa vimefika 89.

Rais huyo ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa la Spiritual Pentecoste Church of Tanzania (SPCT), alitoa ushauri huo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maafa yalitokea Desemba 3, mwaka wilayani Hanang.

Alisema anaipongeza serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ilivyoshiriki kutoa msaada kwa waathirika wa janga hilo kuanzia hatua za awali hadi sasa.

"Ninaipongeza sana serikali kwa jitihada za kuokoa ilizofanya pamoja na kutoa misaada mbalimbali, lakini ipo haja kwa serikali kutumia wataalamu wake kufanya tathmini ya maeneo mengine ambayo ni hatarishi ili kuwaondoa watu kabla ya majanga kutokea na kugharimu maisha yao," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema mbali na Katesh, pia yapo maeneo mengi nchini ambayo wananchi wanaishi, lakini si salama kwa maisha yao.

"Serikali ione namna ya kutumia wataalamu wake kuwaondoa wote ambao wanaishi kwenye maeneo hayo ikiwamo mabondeni na kwenye njia za maji ili adha kama hii isijitokeze tena," alishauri.

Alisema serikali kupitia wataalamu wake inapaswa kutoa ushauri na elimu kwa wananchi kujenga makazi ya kuishi katika maeneo salama.

"Serikali kupitia wataalamu wake inapaswa kutoa ushauri kwa wananchi maeneo salama kwa ajili ya kujenga makazi yao badala ya kuwacha halafu baadaye yanawakuta kama haya yaliyotokea Hanang," alitahadharisha.

**Rais huyo ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa la Spiritual Pentecoste Church of Tanzania (SPCT), alitoa ushauri huo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maafa yalitokea Desemba 3, mwaka wilayani Hanang.**

Aliwataka viongozi wa kisiasa nchini kuwa kitu kimoja kila yanapotokea majanga kama hayo ya kitaifa na kuacha itikadi za vyama vyao.

"Majanga kama haya ni mambo ya kitaifa, kila mtu yanamhusu, hivyo wanasiasa lazima wawe kitu kimoja ili kusaidia waathirika bila kujali itikadi za vyama vyao," alisema.

Aliwataka viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa kuondokana na majanga kama hayo pamoja na majeruhi kupata nafuu haraka ili kurudi katika shughuli zao za kila siku za kujipatia kipato.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki iliyopita kuhusu tukio hilo, alisema hadi sasa watu walipoteza maisha katika tukio hilo ni 89 na majeruhi 14 walikuwa hospitalini.

**KABWELA** Fadhili Mohamed



# RC aonya TRA uonevu katika kodi

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amewataka watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kujiepusha na vitendo vya rushwa na kuwakandamiza wafanyabiashara kupitia kivuli cha cheo.

Pia ameonya watu wanaokahidi kulipa kodi kwamba watawachukulia hatua za kisheria.

Chalamila aliyaelekeza hayo jana mkoani Dar es Salaam alipokutana na watumishi hao kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali yatakayoboresha utendaji kazi, ikiwamo kueleza changamoto na fursa zilizopo.

Kiongozi huyo alisema kazi wanayofanya ni yenye lawama na ni vyema wasiogope kwa kuwa ndiyo maisha yao.

"Msiogope lawama zipo, kuna watu wanalipwa mshahara kwa kulaumu, msipolielewa hilo mtapata shida, kwa sababu kazi yako kubwa ni ya kulaumiwa," alisema.

Alisema kila mtumishi wa TRA anapaswa kutambua nafasi yake kwa kujenga misingi ya uadilifu, weledi, uwajibikaji na kuaminika.

Alisisitiza kuwa mtumishi wa TRA anapolaumiwa hata yeye inamhusu, akionya kwamba kuletwa Dar es Salaam kufanya kazi haina maana ujigambe au uone kama umepandishwa cheo.

"Huu ndio mkoa 'potential' (muhimu) wa kikodi, walipakodi wake ni wengi na wawekezaji ni wengi. Kuna vitu vingi kama bandari, uwanja wa ndege, soko kubwa la Kariakoo, vyote hivi kwa pamoja vinachangia kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali.

"Kama mnakutana na mambo ya kisiasa katika ufanyaji kazi wenu, hilo tuachieni sisi, hivi vitu haviendi pamoja ni kama uchanganye 'flagyl' na pombe, sisi tutawasaidia kuwabana.

"Na akikuletea uchonganishi kwa Rais Samia Suluhu Hassan na wananchi, tutakutetea tutamwambia mama achana na huyo mtumishi, huyu mfanyabiashara ndio msumbufu kulipa kodi," alisema Chalamila.

Alisema ataendelea kuwa mkali pale panapotokea mkwamo katika ulipaji kodi kwa kuwa fedha zinazotokana na kodi ndizo zinazosaidia kuendesha nchi na miradi yake ya kimkakati.

Aliagiza TRA kuendelea na utoaji wa elimu kwa mlipakodi katika maeneo yote yenye biashara za kimkakati, akiahidi kuwapa ushirikiano.

"Tunapoelekea kwenye uchaguzi, kuna maneno mengi yanaweza kuwakatisha tamaa, kila mnapogusa mtaambiwa tunajiandaa na uchaguzi, kazi yenu inahusiana na siasa lakini si kwa mtazamo huo.

"Ukiona unakwenda sehemu kukusanya kodi halafu unakutana na vitisho usimfanye chochote, hapo inabaki kazi ya Jeshi la Polisi kumfuata na kukusogezea ofisini kwako alaah... ndio hii ni kujiepusha na jinai maana mfanyabiashara akifia mkononi mwako itaonekana TRA imeua kumbe pengine mtu mwenyewe alikuwa ameshajifia," alionya.

Chalamila alisifu ufanyaji kazi wa mamlaka hiyo katika Mkoa wa Dar es Salaam, akidai wana ushirikiano mkubwa.

Mkuu wa Wilaya Kinondoni, Saad Mtambule, aliahidi kushirikiana na maofisa hao katika kutoa elimu ya hamasa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Pia alisema watashauriana kuangalia namna bora itakayomfanya mfanyabiashara akiuza atoe risiti na mnunuzi akinunua adai risiti ili kuepusha upotevu wa kodi.

Naibu Kamishna wa Kodi za Ndani Walipakodi Wadogo, Edmund Kawamala,

alisema kodi ni nyenzo muhimu ya uwekezaji, hata kwa vizazi vijavyo kwa kuwa maendeleo yake yataacha alama.

"Ukichukululia mfano daraja la juu la Ubungo limejengwa kwa kodi, litadumu hata miaka 100, wajukuu zetu wa baadaye tukiwaonesha watasema kuna watu walilipa kodi likajengwa.

"Pamoja na kukusanya kodi lazima tuzingatie haki za walipakodi, mlipakodi anayo haki ya kudhaniwa ni mwaminifu na kuheshimiwa, lakini anapaswa kulipa kodi kwa wakati na kutoa taarifa kamili kwa TRA," alisema.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Theopista Mallya, akizungumza na wanakijiji wa Hangomba wilayani Mbozi ambao wametakiwa kuachana na imani potofu za kishirikina ikiwamo ramli chonganishi na unywaji wa pombe uliopindukia. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

# Tanzania yavuna kampuni 56 COP28

**Na Mary Geofrey**

TAASISI na kampuni 56 kutoka mataifa mbalimbali duniani, zimejitokeza kushirikiana na sekta binafsi nchini kuwekeza kwenye eneo la mabadiliko ya tabianchi.

Hatua hiyo ni manufaa ya Mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu kuanzia Novemba 30 hadi Desemba 12, mwaka huu, ukihusisha washiriki 400 kutoka Tanzania, wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa Tanzania kwenye COP28 na manufaa yake.

Alisema kupitia mkutano huo, wawekezaji wa Tanzania walikutana na wawekezaji kutoka nje ya nchi na kujadiliana kuhusu fursa za uwekezaji kwenye eneo la mabadiliko ya tabianchi na kupata kampuni na taasisi hizo 56 zilizovutiwa kuwekeza.

"Kupitia mkutano wa COP28, Tanzania itanufaika zaidi na fedha za miradi, teknolojia, utaalamu na programu mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo programu ya Afrika ya Nishati Safi ya Kupikia, Programu ya Afya na Mabadiliko ya Tabianchi na utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha uhimili katika katika sekta ya maji, misitu na bahari," alisema.

Waziri Jafo pia alibainisha kuwa kutatua changamoto ya matumizi ya nishati ya kupikia kwa wanawake barani Afrika, kunahitaji uwekezaji wa Dola za Marekani bilioni nne kila mwaka.

Alisema kila nchi wamekubaliana kuweka mikakati ya kushirikiana na sekta binafsi kusambaza nishati mbadala katika maeneo yote ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema pia wameweka mikakati ya kukusanya Dola za Marekani bilioni 1.8 kwa ajili ya kuchimba visima 65,000. Kila kisima kitatoa huduma kwa wakulima 16 wenye mashamba ya ukubwa wa hekta 2.5.

Dk. Jafo alisema pia wamekubaliana malengo 11 ikiwamo uendeshaji mfuko wa kukabiliana na upotevu na uharibifu utokanao na mabadiliko ya tabianchi na uundwaji wa bodi ya ushauri ya mfuko huo.

Vilevile, alisema wamekubaliana kuwapo mfumo wa masoko na usio wa masoko wa biashara ya kaboni. Nchi zimesisitiza kuimarisha zaidi mikakati ya taifa ya upunguzaji gesi joto na kuimarisha misingi ya matumizi ya soko.

Dk. Jafo alisema nchi zinazoendelea zinatakiwa kujengwa uwezo kuhusu mfumo wa utoaji taarifa za jitihada zinazochukuliwa katika nchi husika za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo matumizi ya mfumo wa uwazi wa utoaji taarifa za misaada inayotolewa kwa nchi hizo.

Alisema pia wamekubaliana kuimarisha utekelezaji hatua za kupunguza uzalishaji gesi joto katika matumizi ya teknolojia na mbinu za asili ikiwamo utunzaji mfumo ikolojia ya misitu, bahari na milima vinapaswa kuimarishwa.

Alisema imeanzishwa programu ya vijana ambayo inatambulika chini ya utaratibu wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ambapo vijana wenye umri wa kati ya miaka 18 na 35 watateuliwa kuendesha majadiliano kwa ajili ya kuimarisha ushiriki wa vijana katika shughuli za mabadiliko ya tabianchi.

## Serikali yaahidi ushirikiano kukabiliana na ujangili nchini

**Na James Kandoya**

SERIKALI imeahidi kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kuendeleza uhifadhi wa wanyamapori na kukomesha ujangili.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori na Mpango wa Usimamizi wa Tembo Tanzania 2023-2033 uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huo ulifanywa na wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) na wadau wengine wa maendeleo wanaojihusisha na uhifadhi wa wanyamapori.

Alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali ya uhifadhi wa wanyamapori, na kwamba mbinu zinazotumika zitaongeza watalii kufikia zaidi ya bilioni tano mwaka 2025 na kuingiza kipato cha zaidi ya Dola za Marekani bilioni sita.

"Hatuwezi kuwa na utalii imara bila kuweka mkakati mzuri wa uhifadhi wa wanyamapori," alisema.

Alitoa wito kwa sekta binafsi na wadau wanajenga hoteli za kutosha ili watalii wapate sehemu nyingi za kulala.

Takwimu za hivi karibuni za wizara za 2022 zinaeleza kuwa tangu mwaka 2014 Tanzania imekuwa na ongezeko la tembo kutoka 43,330 hadi 60,000 na faru ikifikia zaidi ya 200.

Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Shigeki Komatsubara, alipongeza Tanzania, wadau wa utalii na wananchi kwa jitihada za kupambana na ujangili nchini.

Mradi wa IWT ni kichocheo cha mabadiliko chanya, yanayoonyesha umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kuhifadhi wanyamapori na kuongeza kuwa UNDP itaendelea kuisaidia Tanzania katika kuendeleza juhudi zake za kupambana na ujangili.

"UNDP inasimama pamoja serikali na washirika wake katika vita vya kupambana na ujangili na kulinda hazina ya Tanzania kwa vizazi vijavyo. Tutaendelea kusaidia nchi katika kuendeleza juhudi zake dhidi ya ujangili," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Wilbard Chambulo, alisema sekta binafsi iko tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha sera iliyozinduliwa inatekelezwa vizuri ili kukuza utalii nchini.

"Hadi sasa utalii wa Tanzania uko mbali sana hakuna nchi yoyote za jirani zinazoweza kutufikia kutokana na vivutio vyetu vya kipekee," alisema na kuongeza kuwa juhudi za pamoja zitasaidia kuongeza idadi ya watalii nchini.



## Wasomi wapongeza kasi kukua uchumi wa nchi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATAALAMU wa uchumi wamesema kuwapo kwa fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye sekta za viwanda, biashara na kilimo kumechochea kuongezeka kwa kasi ya kukua kwa maendeleo ya uchumi ukilinganisha na nchi ya Afrika Kusini.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati wa mkutano wa uchumi shirikishi kwa jamii ili kuhamasisha vijana kulinda na kunufaika na uchumi wao, Dk. Cairo Mwaitete, alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na fursa nyingi na kuvutia  wageni kutoka nchi mbalimbali kuja kuwekeza.

Alisema pamoja na ukuaji wa kasi wa uchumi  kwa asilimia saba kwa kipindi cha miaka 10 bado tunatakiwa kuwaandaa vijana ili wawe na uwezo wa kuanzisha viwanda na biashara kubwa kuchochea zaidi ukuaji wa uchumi.

"Hapa nchini kuna fursa nyingi mno kwenye maeneo ya malighafi, viwanda, uchimbaji wa madini na kilimo hivyo tunataka kuona Watanzania wanamiliki mashamba makubwa na kulima, tunataka tuwaone watu wetu wakichimba na kuuza madini nje ya nchi pamoja na kuanzisha viwanda vikubwa," alisema.

Vilevile alitoa rai kwa watunga sera kutunga ambazo zitakwenda na wakati hasa kwa kuangalia mazingira ambayo yanahitaji mashirika na taasisi binafsi ziweze kusimamiwa na Watanzania wenyewe badala ya watu kutoka nje ya nchi.

"Niaomba watunga sera kupitia na kuangalia sera ziwe za ushirikishaji wa kijamii wa uchumi shirikishi ambao utaleta matokeo kwa mtu mmoja mmoja ili kuongeza pato la taifa," alisema.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuwahamasisha vijana kujifunza namna ya kuingia kwenye uchumi, wawe na ujasiri wa kuanzisha viwanda, biashara kubwa na kuingia kwenye kilimo na kutambua fursa zinazoizunguka nchi hiyo.

Mkurugenzi wa Utafiti, Ushauri na Machapisho, kutoka Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Dk. Mordecai Matto, alisema katika mkutano huo wamekutana na wadau kujadiliana namna ya kufikia uchumi shirikishi na changamoto zinazowakabili katika jamii.

Alisema kwa sasa tafiti nyingi zinazofanyika duniani zinajikita zaidi kwenye utafiti wa uchumi shirikishi unaogusa watu wote kwa kuwa maendeleo yasipomfikia mtu mmoja mmoja kunakuwapo kwa changamoto kwenye nchi.

# OSHA yapewa jukumu kusajili maeneo ya kazi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), umeagizwa kusajili maeneo yote ya kazi nchini pamoja na kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanapatiwa miongozo ya namna ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya magonjwa na ajali hadi kufikia Juni 2024.

Agizo hilo, limetolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),Cyprian Luhemeja,alipokuwa akizindua Baraza la Tano la Wafanyakazi wa OSHA Jijini Arusha.

Mhandis Luhemeja, alisema OSHA imepewa dhamana ya kujenga nguvukazi salama na yenye afya njema kwa maendeleo endelevu ya Taifa na hivyo ni lazima Taasisi hiyo itimize wajibu huo ipasavyo.

"OSHA ni taasisi yetu ambayo imepewa jukumu la kusimamia Sheria namba tano ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ambayo serikali yetu kupitia Bunge iliitunga na kuunda chombo mahsusi ili kiweze kusimamia sheria hiyo kwa manufaa ya Watanzania," alisema Luhemeja.

Alisema usalama na afya mahali pa kazi ni muhimu sana kwa sababu dunia inabadilika ndio maana wameipa OSHA jukumu la kusimamia wafanyakazi wasipate matatizo ya kiafya wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa baraza hilo, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema taasisi yake imeyapokea maagizo ya Katibu Mkuu na itayatekeleza ipasavyo.

Alisema kikao cha baraza hilo kinategemea kufanya tathmini ya utendaji wao kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na nusu ya kwanza ya mwaka 2023/2024 kujadili namna bora ya kutekeleza maagizo tuliyopewa pamoja na kuendelea kuboresha utendaji wa taasisi hiyo.

Uzinduzi wa Baraza hilo umefanyika sambamba na uchaguzi wa viongozi pamoja na wajumbe wa Kamati Tendaji wake ambapo viongozi mbali mbali walihudhuria wakiwemo Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Comrade Heri Mkunda, Kamishna wa Kazi, Suzan Mkangwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Mkoa wa Dar es Salaam, Sarah Rwezaura.

Katibu Mkuu wa TUCTA ambaye ni Katibu Mkuu wa TUGHE, Comrade Mkunda, aliipongeza OSHA kwa kutekeleza ipasavyo Mkataba wa Mabaraza ya Wafanyakazi na hivyo kuwa kati ya taasisi 20 zenye mabaraza bora nchini.

"Ni utaratibu wa kisheria kwamba taasisi zote lazima ziwe na mabaraza ya wafanyakazi ili kutoa fursa kwa wafanyakazi kushiriki katika uamuzi muhimu unaoihusu taasisi yao kwani wafanyakazi ndio wamiliki wa Taasisi. Nitoe rai kwa waajiri wengine kuhakikisha mabaraza ya wafanyakazi yanakuwepo na yanafanya kazi ipasavyo kama ilivyo kwa OSHA na taasisi nyingine zinazofanya vizuri," alisema.

OSHA ni Taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 iliyoundwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba taratibu muhimu za kulinda afya na usalama wa wafanyakazi zinazingatiwa ipasavyo.




Mwenyekiti wa Mtandao wa Wakulima mkoani Manyara (MVIWAMA), Paulo Joseph (katikati), akizungumza kuhusu kilimo ikolojia kwenye Mkutano Mkuu wa 16 uliofanyika mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wahitimu IAA wakumbushwa kutumia matokeo ya utafiti kutatua changamoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Kilimo, David Silinde, amewaelekeza wahitimu wa kozi mbalimbali katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), kutokufungia ndani matokeo ya utafiti waliofanya badala yake, watumie matokeo hayo kutatua changamoto zinazoikabili jamii inayowazunguka.

Akizungumza katika mahafali ya 25 ya chuo hicho kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwingulu Nchemba, Silinde alisema kila mhitimu anapaswa kutumia vizuri matokeo ya utafiti alioufanya na kushirikisha jamii husika kutatua baadhi ya changamoto.

"Msifungie matokeo ya utafiti wenu baada ya kuhitimu, yatumieni, shirikisheni jamii ili yaweze kuwa chachu katika kuleta mabadiko chanya, kuongeza tija kwenye shughuli za kiuchumi na utendaji kazi wa kila siku, usimamizi wa taasisi na mashirika, uboreshaji wa sera pamoja na mipango na mikakati kwa maslahi mapana ya taifa letu," alisema Silinde. Aidha, aliwahimiza kuendelea kujifunza, kufanya kazi kwa bidii na kuwa raia wema kwa jamii na taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kutafakari namna watakavyotumia elimu waliyoipata kupambana na umasikini na kuleta maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

"Serikali, wazazi, walezi na wafadhili wenu tuna matumaini makubwa nanyi kwamba uwekezaji tuliofanya kwenye elimu yenu haikuwa bure, bali matokeo na tija ya elimu mliyoipata yataonekana dhahiri kwenye mchango wa kila mmoja katika maendeleo ya uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alieleza.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema wanatoa kozi 71na kati ya kozi hizo 16 ni ngazi za shahada,17 ni stashada, 24 astashahada na kwa upande wa uzamili wana kozi 14.

Alisema wanaendelea na uhuishaji wa mitaala ili kuhakikisha chuo kinatoa kozi ambazo zinaendana uhalisiana mahitaji ya soko na kuwa mpango mkakati wa chuo hicho, kwa miaka mitano ni kuendelea kupanua wigo ndani na nje ya nchi ukiacha kampasi nne walizonazo ikiwemo ya Arusha, Dar es salaam, Dodoma na Babati.

Pia alisema tayari wana eneo la serikali na limeshatengewa bajeti ya takribani Shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha ujenzi wa kampasi mpya ya Songea.

"Kwa Dodoma kwa kutumia fedha zetu za ndani tumeshaanza kujenga jengo ambalo litaweza kukalisha wananfunzi 4500 kwa mara moja lakini pia kimataifa tumefanya mikakati mbalimbali ikiwemo ziara Sudan ya Kusini na tupo tayari kuanzisha campus ya kwanza nje ya nchi katika mwaka ujao wa masomo," alisema Prof Sedoyeka.

Alisema kwa kampasi za Ruvuma na Babati zimejikita katika uchumi wa kati ikiwemo shughuli za kilimo, ufugaji, usindikaji, utalii na kuendelea kutoka na ndio ukweli na uhalisia wa maeneo hayo ambapo pia wameanzisha ushirikiano na chuo cha Polisi Moshi kwa kuanza kutoa kozi mbalimbali zinazolenga ulinzi na usalama.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa IAA,CPA Joseph Mwigune, alisema katika mahafali hayo wamehitimu jumla ya wanafunzi 5387 ambapo katika ngazi ya shahada ya uzamili wana wahitimu 1139, ngazi ya shahada 1027,ngazi ya Stashahada 1260 na ngazi ya Astashahada 2061.

"Chuo kimeendelea kutoa elimu kwa kupitia wataalamu mahiri, miundombinu bora na rafiki inayoendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na mitaala bora inayowaandaa wanafunzi mahiri wenye ujuzi na maarifa yanayohitajika wakati wa sasa na ujao," alisema.



# Ongezeko kina Ziwa Viktoria laathiri makazi, mazao Chato

**Na Daniel Limbe,** CHATO

KUONGEZEKA kina cha maji katika Ziwa Viktoria kumesababisha athari kwa wakazi wa Wilaya ya Chato, mkoani Geita ikiwamo nyumba, mazao pamoja na miundombinu kuvamiwa na maji hali inayorudisha nyuma shughuli za maendeleo.

Hali hiyo imetajwa kusababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha wilayani hapa huku baadhi ya wakulima wenye mashamba kando ya ziwa wakieleza kupata hasara kutokana na mazao yote kusombwa na maji.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti waathirika wa ongezeko hilo la maji walitaja nyumba zao kuzingirwa na maji hali inayowalazimu kukimbia makazi yao kwa muda.

Mmoja wa waathirika, Consolata Maganga alisema tangu ajenge nyumba hiyo miaka miwili iliyopita hajawahi kukutana na hali ya hiyo lakini mwaka huu maji ya ziwani yamefika katika nyumba yake na kulazimika kutafuta hifadhi na kuhama.

"Kwa sasa ninapanga eneo la jirani ili kunusuru maisha yangu na familia yangu na cha kushangaza wakati nanunua eneo hili hakukuwa na dalili kuwa maji yanaweza kujaa na kufika hapa nilipo," alisema Consolatha Maganga.

Mkulima Sara Ponsian alisema amekuwa akiendesha kilimo cha mazao mchanganyiko ikiwamo viazi vitamu, maharage, mahindi, miwa na kunde lakini msimu huu amepata hasara kubwa baada ya shamba lake kujaa maji na mazao yote kuharibika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chato, Makonzele Phinias, alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakiuziwa maeneo ambayo hayafai kwa ujenzi wa makazi na wengine kuendesha shughuli za kilimo kwenye maeneo yaliyo karibu zaidi na ziwa.

"Tatizo kubwa la wananchi wetu ni kutoamini kama maji yanaweza kurejea yalipowahi kukaa, siku za nyuma maji yalipoonekana kupungua ndani ya ziwa baadhi ya watu waliongeza ukubwa wa mashamba yao kwa kuyafuata."



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (kushoto), akipata maelekezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kituo cha Rasilimali za Kilimo Kata ya Mondo, Michael Emmanuel (kulia) juzi, jinsi wanavyokausha embe, mchicha na bamia, ambapo kilo moja ya unga wa mchanganyiko huo unauzwa kwa Sh.30,000, kituo hicho kinafadhiliwa na Mgodi wa Buzwagi, wilayani Kahama. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mfawidhi alia na ubovu wa barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Luzila John, amelalamikia ubovu wa barabara inayoelekea hospitalini hapo kuwa unahatarisha maisha ya wagonjwa na wajawazito wanaoitumia mara kwa mara.

Dk. John alitoa kilio hicho juzi katika Kikao cha Kamati cha Ushauri mkoani Shinyanga (RCC) kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Christina Mndeme na kutaja kipande hicho chenye urefu wa kilometa nne kutokuwa rafiki kwa safari za wagonjwa.

Alisema kipande hicho kimekuwa kiki hatarisha maisha ya wagonjwa na kuiomba serikali iijenge kwa kiwango cha lami kutokana kuwa na umuhimu mkubwa katika kuwafikisha wagonjwa hospitalini hapo kupata huduma.

"Hivi karibu gari la wagonjwa lilipata ajali kwenye barabara hiyo na kupasuka taili na siyo mara ya kwanza kwani magari yamekuwa yakiharibika mara zote tunaomba ijengewe kwa kiwango cha lami," alisema Dk. John.

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini Patrobas Katambi, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira, Vijana na watu wenye ulemavu, alikumbushia kuwa matengenezo ya kipande hicho ni ahadi ya Makamu wa Rais Dk. Philipo Mpango na kusikitishwa hadi sasa haijatekelezwa.

Meneja Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) mkoani Shinyanga, Mhandisi Oscar Mlekwa, alisema barabara hiyo tayari ipo kwenye mpango wa matengenezo kupitia mradi wa kuboresha miji (TACTIC) kwa ufadhili wa benki ya dunia na itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliwaagiza TARURA wakaifanyie matengenezo kipande hicho kwa kuweka changarawe ili ipitike vizuri na kutohatarisha maisha ya wagonjwa wakati wakiendelea kusubiri mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami.

# Mil. 976/- kunoa wakulima uzalishaji mazao bora

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MRADI wa Kituo cha Rasilimali za Kilimo wenye thamani ya Sh. milioni 976 umeanza kuwanufaisha wakulima kutoka kata mbili za Mwendakulima na Mondo zilizoko katika Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, kupitia elimu ya uzalishaji wa mazao ili kuboresha kilimo.

Utekelezaji wa mradi huo ambao upo chini ya Mgodi wa Barrick-Buzwagi ulianza mwaka 2018 ili kuwawezesha wakulima kulima kisasa katika kilimo cha biashara na chakula.

Ofisa uhusiano wa Mgodi huo, Yunia Wangoya, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema, uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara umeongezeka kulinganisha na ilivyokuwa hapo awali.

Alisema, vituo hivyo vimegharimu Sh.milioni 976.5, kati ya hizo Sh.milioni 30 ni gharama za ardhi iliyotolewa na Halmashauri hiyo huku Sh.milioni 946.5 ikigharamia ujenzi wa miundombinu ya mifumo kwa wakulima.

Alitaja kaya zilizofikiwa na kupatiwa elimu ya kilimo bora kupitia mashamba darasa ya mahindi, alizeti na mpunga kuwa ni 4,648 huku uzalishaji wa mazao ukiongezeka kwa zaidi ya tani mbili. "Kwa mahindi awali walikuwa wakipata tani 1.5 kwa heka ila sasa wanapata tani 3.5, mpunga kutoka tani mbili hadi tani 3.5 huku Alizeti wakipata tani 3.5 tofauti na awali ambapo walikuwa wakipata tani 0.8. Mradi huu utasaidia kukabiliana na ukosefu wa chakula kwenye maeneo husika," alisema Wangoya.

Vilevile alisema kupitia mradi huo wakulima wamepatiwa trekta ya kilimo, mashine za kusaga, kukoboa mpunga, kugredi na kukamua mafuta ya alizeti hivyo kumhakikishia kuwa mafuta safi ya zao hilo yanapatikana katika kata hizo za Mondo na Mwendakulima.

Meneja wa Mgodi wa Buzwagi, Rebecca Stephen, alisema, mradi huo utakuwa endelevu kwani mpaka sasa jumla ya vyama vya msingi viwili vyenye wanachama 246 vimesajiliwa na ndivyo vitakavyosimamia mradi kwa kushirikiana na maofisa ugani wa kata na kuwataka kuzingatia mafunzo wakati wa uzalishaji shambani.

Mmoja wa wakulima hao, Rosemary Samweli alisema, kupitia mradi huo ameongezewa ujuzi wa kulima kisasa kama vile uvunaji wa kisasa ili kuondokana na upotevu wa mazao shambani, kuepuka sumukuvu kwenye mazao hasa mahindi na uzalishaji umeongezeka kwa hekari moja.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliupongeza uongozi wa Barrick Buzwagi kwa kuanzisha mradi huo ili kuwanufaisha wakulima na kuongeza tija na uzalishaji katika mazoa ya chakula na biashara kabla ya kukamilisha taratibu za ufungaji wa mgodi.

Aidha, aliwashauri wakulima kuutumia mradi kukua kiuchumi na kuwaelekeza wakurugenzi wa halmashauri za mkoa kuiga mfano huo na kuanzisha vituo vya namna hiyo kwenye maeneo yao ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kibiashara.




Ukurasa 12

**Wakati wataalamu wanatumia 'kidigiti' kwa wanajamii ni 'kidijitali'**







Ukurasa 13

Hizi ni chache kati ya maelfu ya faida za viungo vya chakula



Ukurasa 14

MADAI WANAWAKE KAMBI ZA WAVUVI

**Kulazimishwa kuwa na mabwana, kutumikishwa kambini bila malipo**

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 19, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

HITIMISHO SIKU 16 VS UKATILI KIJINSIA

# Wilaya tishio unyanyasaji kwa Zanzibar ni hizi hapa



Wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WIKI mbili za Kampeni ya Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zilizoanza Novemba 25 na kuhitimishwa mwanzoni mwa Desemba zinazinyooshea vidole wilaya tatu vinara kwa ukatili na unyanyasaji Tanzania Visiwani zikitajwa kuwa, ni Magharibi A, Magharibi B na Wilaya ya Mjini.

Aidha, Jeshi la Polisi visiwani nalo halijawekwa pembeni, linaagizwa kuharakisha upelelezi wa kesi za ukatili wa kijinsia ili zimalizike kwa wakati na kupunguza kero na malalamiko,, ni maagizo ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, wakati wa kuhitimisha kampeni ya Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zilizoanza Novemba 25 hadi Desemba 10.

Akiagiza juhudi zifanyike kukomesha vitendo vya ukatili kisiwani, wilaya vinara katika unyanyasaji ni Magharibi A yenye matukio 253, Magharibi B visa 288 na Mjini matukio 253 na kwamba wenye ulemavu wanakumbana na vitendo hivyo.

Taarifa za Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinaonyesha kuwa hali inatisha, kwani kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu matukio 1,620 ya ukatili yameripotiwa.

" 1,360 kati ya hayo ni ya watoto, 194 wanawake na 77 ni wanaume, wakati 651 kati ya 1,620 ni ya kubaka, 200 ya kulawiti, 88 kuingilia kinyume na maumbile, 84 kutorosha, 125 kukashifu na 212 shambulio la aibu," anasema Riziki, akinukuu taarifa za mtakwimu wa serikali.

Anasema, Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa, lakini bado kuna ucheleweshwaji wa upelelezi wa kesi hizo hali inayosababisha nyingi kukaa muda mrefu katika vituo vya polisi Zanzibar.

"Kuendelea kwa hali hii kunaweza kuathiri lengo la serikali la mapambano ya kuondoa vitendo hivyo kwa kuwatia hatiani watu wanaothibitika kufanya ukatili ndani ya jamii," anasema.

Aidha, Waziri Riziki anasema, umefika wakati wa kufanya tafakuri ya kina kwa ajili ya kuwakomboa waathirika wa matukio hayo yanayotokea ndani ya jamii, wakiwamo watu wenye ulemavu.

"Ni muhimu wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia kuelekeza nguvu katika kampeni ya 'Wekeza katika Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watu Wenye Ulemavu na Nijuze Nijilinde Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia," anasema Waziri.

Usawa wa kijinsia utakuwa na tafsiri nzuri iwapo kila mtu atatendewa haki kwa mujibu wa sheria, mila na silka ya Zanzibar kwa makundi yote ndani ya jamii.

Waziri anazungumzia mkakati wa wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, unavyolenga kupitia na kuandaa mpango kazi mpya wa kitaifa wa kupambana na ukatili na udhalilishaji kwa wanawake, watoto na wanaume katika ujumuishaji wa shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2023 hadi 2027.

Ili kufanikisha mpango huo, anawaomba wananchi, wataalamu wa kada mbalimbali kuendelea kutoa maoni yao yatakayofanikisha uandaaji na utekelezaji wa mpango kazi huo, watakapohitajika kufanya hivyo kuptia timu ya wataalam waelekezi.

Kadhalika, anapongeza kazi inayofanywa na wana wanazuoni wakiwamo viongozi wa dini ambao ni muhimili mmoja wa wanajamii katika kusimamia uamrishaji mwema na kukataza maovu ndani jamii.

"Kazi mnazofanya zinasaidia serikali kuyafikia malengo yake, hivyo niwaombe muendelee na kazi ya kuelimisha jamii iondokane na ukatili na udhalilishaji kwa vizazi vya sasa na baadae," anasema.

Anasema ni jukumu la wote kuendeleza kutoa elimu kuhusu athari za ukatili wa kijinsia, ili jamii ipate uelewa wa kutosha wa ubaya wa vitendo hivyo.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Abeda Rashid Abdalla, anasema matukio ya udhalilishaji yanaongezeka ikiwamo matukio ya kubaka, kunajisi,a kwamba wilaya ya Mjini na Magharibi B zinaongoza

"Ni vyema jamii kuanzia wanaumme na wanawake kupambana na matendo hayo, kwani bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuyapondoa ndani ya jamii yetu," anasema Abeda.

Katibu Tawala Mkoa wa Kusini Unguja, Radhia Rashid Haroub, anaishukuru wizara kwa kuufanya mkoa kuwa kuwa mwenyeji wa kilele cha maadhimisho ya Siku 16 ya kampeni ya kupinga ukatili.

"Mapambano yaliyopo, yanahitaji nguvu zaidi, kwani mkoa huu matukio hayo yanaongezeka. Mwaka jana yalikuwa 1,320, mwaka huu yamefikia matukio 1,620 sawa na ongezeko la asilimia 16,"anasema Radhia.

Anaomba wizara kuja na mkakati utakaoweka misingi mizuri ya kupinga vitendo hivyo hasa kwenye, kwa kuwa matukio mengi ya aina hiyo yanatokea ndani ya familia.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

UTATA WA KUTOHOA

# Wakati wataalamu wanatumia 'kidigiti' wanajamii ni 'kidijitali'

KUTOFAUTIANA katika kupata tafsiri sahihi za maneno ya Kiswahili zitaendelea mradi maneno yanahitaji kusanifiwa au kukubaliwa ili yatumike rasmi. Ila maneno kwa jumla yanaanzia mitaani halafu wenye taaluma hiyo wanajitahidi kuyasanifu, iwe ni kwa kutumia kanuni halisi za usanifu au ni kufuatilia jinsi yanavyotamkwa katika jamii.

Mara moja moja katika vyombo vya habari kuna ubishi unazuka kuhusu neno hili au lile, kwa kuwepo njia moja ya kutamka au kuandika inayotumiwa zaidi kijamii, na mwelekeo wa kitaaluma unaokosoa matumizi, kutaka kufanya marekebisho.

Katika mijadala kama hiyo wanataaluma wanashinda kwani ina mfumo wa kuinua suala linalohusika na kulijadili, halafu kulitamatisha, na wasikilizaji au wachangiaji wanaopiga simu wanakuwa na nafasi finyu ya kubadilisha mwelekeo wa mjadala. Mzungumzaji kutoka taasisi ya kitaaluma kama Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) atakuwa ndiye aliyekaribishwa kufafanua suala hilo, na siyo rahisi kwa nafasi hiyo itokee 'azidiwe nguvu' na mchangiaji halafu tamati ya hoja ielekee kwingine ni vigumu. Kufikia hali hiyo ni kama kuashiria mabadiliko hata katika taaluma yenyewe, kutokana na jamii.

Mfano mmojawapo ni matumizi ya neno king'amuzi tofauti na kisimbusi, neno ambalo 'linatambuliwa' na BAKITA au kusanifiwa kuwa rasmi, wakati ndani ya jamii unaweza kusema king'amuzi inaeleweka zaidi na rahisi zaidi kutumia. Mtaalamu wa BAKITA katika moja ya redio za FM, anaeleza neno kisimbusi 'lilivyotoholewa' (wengine wangesema lilivyoundwa au lilivyobuniwa).

Kigezo cha msingi katika ubunifu huo ni kutofautisha kung'amua 'detect,' yaani kugundua, halafu 'msimbo' kana mpangilio wa mistari halafu chombo kinachotofautisha baina ya viashiria hivyo kinakuwa 'kisimbusi.'

Tatizo la tafsiri hiyo ni kuwa inalazimisha maana moja kwa takriban kila neno, hivyo ikitokea tafsiri inafanana na neno lingine, kunakuwa na nafasi ya 'kutohoa' neno jingine, wakati king'amuzi kingeweza kuwa na maana mbili




> Mwelekeo upi utashinda hadi sasa si rahisi kusema, lakini kinadharia chenye uwezo wa kuvutia watu wengi zaidi ni kile kinachotumika kwa urahisi zaidi, na siyo kinachohitaji kamusi ili uthibitishe.

au zaidi katika Kiingereza, kama 'detector' kwa upande mmoja na kama 'decoder' kwa upande mwingine.

Neno kugundua kwa mfano linaweza kuwa ni 'ugunduzi' wa kitu kilichopo kama mmoja wa wavinjari wa awali kutoka Ulaya alivyodai kugundua Mlima Kilimanjaro, akaelemisha dunia, kupitia Ulaya, kuwa upo mlima wenye kilele cha barafu unaopatikana karibu na mstari wa Ikweta, wakashangaa. Ugunduzi mwingine ni kitu kilichojificha, kama nadharia, hesabu.

Yako maeneo ambako wanataaluma wanadakiza, watasema wanatohoa neno ambalo tayari limeanza kutumika au limekubalika, kwa mfano 'digital', ambako wataalamu wanapenda neno digiti, na kuna upande nwingine wa mjadala kama matamshi ya Kiswahili liwe digiti au dijiti.

Kiusanifu huo ndiyo mwelekeo wa kikanuni, mfano biology inatoholewa kuwa 'baioloji, baiolojia' kadhalika 'technology' inakuwa 'teknolojia' au teknoloji' ni kwa sababu 'g' inapotoholewa kwa kanuni za Kiswahili inakuwa 'ji' . Ila kidigiti mwelekeo wa matumizi ni tofauti, kwa maana ya kujihusisha katika matamshi na chanzo cha neno hilo ila haitakuwa rahisi kwa wataalamu, ambao hujumuika chini ya tafsiri au hisia, maamuzi ya wanataaluma wenzao, badala ya kutofautiana kijamii, kubadili hilo. Si rahisi kuona jamii ikielekeza hisia zake kutumia neno 'kidigiti, itaendelea na 'kidijitali'

Kwa maana hiyo inaelekea kutakuwa na mikondo miwili ya kutamka na kuandika, mkondo unaozingatia tafsiri kama ilivyosanifiwa, na ile inayoendana na matamshi au matumizi ya kila siku ya lugha, bila kujali wasanifishaji wanasemaje. Suala hapo ni uthabiti wa usanifishaji kama mhimili wa lugha, pale mhimili huo ukitaka watu wajifunze kwao, wakati maneno yanayokana na watu, yanachipuka kama vipaji vingine, kwani kuanza kutumia neno ni ugunduzi vilevile.

Mwelekeo upi utashinda hadi sasa si rahisi kusema, lakini kinadharia chenye uwezo wa kuvutia watu wengi zaidi ni kile kinachotumika kwa urahisi zaidi, na siyo kinachohitaji kamusi ili uthibitishe.

Mfano mwingine wa utohoaji wa ziada usiohitajika ni neno darubini, ambako wataalamu wa BAKITA wanapendelea kutumia kwa maana ya kuvuta vitu vilivyoko mbali vionekane bayana, kwa kukuza taswira zao kuwa kubwa zaidi. Ni rahisi kuona kwamba kuchukua 'sampuli' ya chochote kile kutoka mwili wa mtu au mazingira na kuweka chini ya darubini, katika maabara, inakuwezesha kuona vimelea, virusi, viluwiluwi au chembe viumbe za miundo tofauti hasa zinazosababisha magonjwa.

Ni maana tofauti za darubini, kama 'kiona mbali' na kama 'kiona ndani,' ila wataalamu wa BAKITA hawataki hiyo maana ya pili kwani inawanyima nafasi ya 'kutohoa' neno jingine, waiite hii ya pili kuwa ni 'hadubini,' ndiyo inatumika maabara. Ni neno ambalo halimsaidii mtu kujua kama linaashiria nini, wakati sifa mojawapo na neno jipya ni hitaji la kuunganishwa kirahisi na maneno yaliyopo, hasa yale ambayo tafsiri husika huyaleta karibu zaidi.

Bado hakuna uhakika ni kwa kiasi gani kuundwa kwa maneno katika lugha kutatokana na usanifu rasmi au maneno yataanza kutumika na kuenea bila kuhitaji kuoanishwa na tafsiri sanifu ya neno. Mojawapo ya maeneo yanayotoa uhakika wa lugha sanifu au matumizi kuwa rasmi ni kuwa idara za serikali au sekta ya umma kwa jumla zinao wajibu halisi wa kutumia lugha sanifu na siyo kutumia kama inavyosikika barabarani kama watu wengine. Endapo bado kutakuwa na msukumo wa kuunda maneno kujaza hitaji hili au lile katika kukua kwa maingiliano ya kijamii, kibiashara au kutafsiri zana za teknolojia au hisia nyinginezo, tofauti itakuwepo katika mikondo ya kutafsiri.

Siyo jambo ambalo linaweza kumalizwa kirahisi, hasa kwa sababu wataalamu wa BAKITA wanapenda kuainisha kuwa kinachosanifishwa ndiyo Kiswahili, na matamshi au tafsiri nyingine ni makosa. Kitakachoeleweka baadaye ni kuwa lugha inakuwa na mikondo tofauti kutokana na kuwa na vianzio maridhawa, na hata katika taasisi za nchi, pale tofauti na matumizi ya umma ikiwa bayana ndiyo ynayofaulu.

Ndiyo maana hakuna mahali utasikia matumizi ya teknolojia ya kidigiti, au kidijiti, ila teknolojia ya kidijitali, au kidijitali. Tofauti hii ya pili inaelemea zaidi kwa matumizi ya kiasili zaidi ya kidigitali, licha ya kutamkwa kama kidijitali, ila jaribio la kurasimisha 'kidijiti' au 'kidigiti' inaelekea linakwama.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Hizi ni chache kati ya maelfu ya faida za viungo vya chakula







WATU wengi wanapenda chakula chenye viungo angalau tangawizi, vitunguu swaumu na pilipili .

Wapo wanaopenda chai ya viungo, juisi, ubuyu na zama hizi hata mahindi ya kuchoma hutafunwa pamoja na viungo kama ndimu, pilipili na tangawizi vilivyowekwa chumvi.

Inawezekana watu hutumia viungo bila ya pengine kujua manufaa makubwa yaliyomo ndani yake, inaandika makala ya BBC Swahili.

Inatoa mfano wa binzari katika mchuzi kuwa inaweza kukusaidia ubongo kukuza kumbukumbu, pilipili ni tiba lishe inayosaidia kupunguza maumivu, na zafarani inakuongezea nguvu na uwezo wa kufanya mapenzi.

### ZAFARANI

Maua ya zafarani ni kiungo cha bei ghali duniani. Kwa Ni jina la Kiarabu, "za-fran" inamaanisha njano ina rangi ya kuvutia ni yenye ladha ya uchungu kiasi ikielezwa kuwa imejaa vioksidishaji na tafiti nyingi zinaonyesha ina sifa ya kupambana na saratani. Pia inasemekana ni kitu muhimu kwa ubongo wa binadamu.

Baadhi ya tafiti zinaonyesha kuwa ukitumia milligram 30 kwa siku inaweza kusaidia kupunguza unyogovu. Tafiti nyingine zinaonyesha kutumia kila siku kunaweza kuboresha ubongo na kupambana na magonjwa ya kupoteza kumbukumbu, BBC inaeleza.

Utafiti kutoka nchini Iran unaoonyesha kuwa matibabu ya kutumia zafarani kwa mwezi mmoja huwapa nguvu ya kufanya mapenzi wanawake wanaosumbuliwa na msongo wa mawazo.

### BINZARI

Kiungo kingine chenye rangi ya njano ni binzari hiki hutoka kwenye mzizi wa mmea jamii ya tangawizi na kwamba binzari imetumika kwa matibabu kwa karibu miaka 4,000.

Inasifika kuwa inaweza kutibu magonjwa mengi kuanzia, maumivu ya viungo na tatizo la kukosa nguvu za kiume, shukrani kwa unga wake wa njano.

Mwaka 2011, watafiti wa kiharusi katika Kituo cha Matibabu cha Cedars-Sinai, Marekani, waligundua unga wa njano uliweza kutibu kiharusi kwa sungura.

Katika Chuo Kikuu cha Illinois Marekani pia, timu ya watafiti iligundua njia ambayo inaonekana kuwa na ufanisi katika kutibu kansa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na melanoma na saratani ya matiti.

Vilevile, katika vipimo vya maabara katika Chuo Kikuu cha Florida, wanasayansi wanatumia unga wa bizari kuharibu na kupambana na saratani ambayo hugunduliwa kwa watoto.

Aidha, BBC inasema kuna ushahidi kuwa unga wa binzari unaweza kusaidia kubadilisha matatizo ya kumbukumbu. Timu ya Chuo Kikuu cha California, ilichagua kirutubisho kinachopatikana kwa wingi katika unga huo kiitwacho 'theracurmin' kwa ajili ya utafiti wao kwa watu wazima 40 wenye shida ya kumbukumbu.

Washiriki walitumia miligramu 90 mara mbili kwa siku kwa miezi 18. Matumizi hayo yaliwafanya washiriki kuimarika pakubwa kumbukumbu zao kuejea.

### MDALASINI

Ni gome la mti lenye harufu nzuri hutumiwa kwenye vyakula vingi vitamu. Mdalasini una ladha nzuri na umetumika kwa muda mrefu katika dawa za jadi, hasa kutibu gesi tumboni na tatizo la kusaga chakula.

Utafiti unaonyesha mdalasini aina ya casia, unaweza kupunguza viwango vya sukari katika damu kwa watu walio na ugonjwa wa kisukari cha aina ya 2 au mwili kukosa kichocheo cha 'insulin' inayowezesha kuvunja sukari mwilini, ingawa matokeo bado hayajathibitishwa.

Utafiti wa Chuo Kikuu cha Ohio unaonyesha mdalasini una ufanisi zaidi katika kupunguza viwango vya sukari ya damu kuliko hata mlo maalumu.

Harufu ya kupendeza ya mdalasini na ladha yake hutokana na kemikali inayoitwa 'cinnamaldehyde,' ambayo ina uwezo wa kuzuia bakteria na kuvu. Utafiti mwingine unaonyesha kemikali hizo zinaweza kusaidia kuzuia unene.

Pia kuna ushahidi mdalasini unaweza kuboresha ubongo. Utafiti katika Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Rush huko Chicago, Marekani, unagundua kuwa mdalasini ulisaidia panya kujifunza na uliongeza kiwango cha protini inayohusika katika kumbukumbu na kujifunza inayoitwa 'CREB.'

Watafiti wanasema mwili hubadilisha mdalasini na kuunda 'sodium benzoate', ambayo hutumiwa sana kama matibabu ya kemikali kwa majeraha ya ubongo.

Lakini fikiria mara kabla ya kutumia kiasi kikubwa cha mdalasini, una kemikali zinazoweza kuharibu ini hivyo huo ni upande wa pili, inatahadharisha BBC.

### PILIPILI

Pilipili ya kuwasha ilianzia Mexico zaidi ya miaka 6,000 iliyopita lakini imeenea kote duniani, ikitumika kama dawa ya kutuliza maumivu mbalimbali, mfano viungo vya mwili na mishipa ya fahamu.

2015, timu kutoka Chuo cha Sayansi ya Tiba cha China ilifuatilia afya ya karibu watu 500,000 kwa miaka kadhaa. Wale waliokula chakula chenye pilipili mara moja au mbili kwa wiki walikuwa na kiwango cha chini cha vifo kuliko wale ambao hawali pilipili.

Uchunguzi wa Afya na Lishe kutoka China unaonyesha kuwa matumizi ya pilipili pia yanahusishwa na viwango vya chini vya unene wa kupindukia, BBC inaongeza.

Utafiti wa hivi karibuni wa Australia unasema wale wanaokula pilipili wana uwezekano mdogo wa kuwa na shinikizo la damu. Pilipili huongeza uzalishaji wa oksijini katika mishipa ya damu na huilinda dhidi ya kuvimba.

Pia ina uwezo wa kupambana na saratani. Ushahidi unaonyesha pilipili inaweza kusaidia kuzuia saratani fulani kutokea na kuzuia ukuaji wa uvimbe. Inadhaniwa kuwa na uwezo wa kuua seli za saratani ya kibofu cha mkojo.

Hata katika suala la lishe ya kawaida, pilipili ina viwango vya juu vya vitamini A na C. Ikiwa wewe si mpenzi wa pilipili, kumbuka maumivu unayohisi wakati wa kula yatafifia kadiri unavyokula mara kwa mara.

> Uchunguzi wa Afya na Lishe kutoka China unaonyesha kuwa matumizi ya pilipili pia yanahusishwa na viwango vya chini vya unene wa kupindukia, BBC inaongeza.

### TANGAWIZI

Tangawizi inatumika kwa matibabu kwa millennia kadhaa na mzizi huu unatoka katika familia moja na manjano unaelezwa kuwa umetumika tangu karne ya 4 kwa maumivu ya tumbo, kichefuchefu na kuhara.

Wagiriki wa Kale waliitumia kupambana na kichefuchefu.Nguvu yake ya kuponya kichefuchefu inamaanisha kuwa inanunuliwa mara kwa mara na wanawake wajawazito. Wakati huo huo, inajulikana pia kuwa na uwezo wa kusaidia kupambana na saratani.

Jambo la kutia moyo ni ukweli usiojulikana kwamba tangawizi huchochea kutokwa na jasho - hivyo hukufanya kuhisi joto, hasa unapohisi baridi.

Uwezo wa tangawizi wa kupunguza kichefuchefu, ugonjwa wa yabisi na maumivu kwa ujumla unahusishwa na kemikali zinazoitwa 'gingerols.' Inaweza kupunguza kiwango cha sukari kwenye damu na kusaidia kukulinda dhidi ya kisukari cha aina ya 2.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

MADAI WANAWAKE KAMBI ZA WAVUVI

# Kulazimishwa kuwa na mabwana, kutumikishwa kambini bila malipo

SAUTI ya Wanawake Ukerewe (SAWAU), ni shirika linalopambana kutokomeza ukatili wa kijinsia, kusaidia wanawake na jamii kwenye uhimilivu katika kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi. Linafanya shughuli zake visiwani Ukerewe mkoa wa Mwanza, ambako kazi kubwa ni uvuvi.

Visiwani kuna ukatili wa aina mbalimbali unaoshuhudiwa kwenye uvuvi hasa ndani ya kambi za wavuvi na kwenye jamii, anasema Sofia Donald, mwasisi wa SAWAU anapozungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, kuhusu kazi za shirika lake kwenye kufikia jamii yenye usawa na ulinzi wa mwanamke na mtoto.

Katika mahojiano maalumu Mkurugenzi wa SAWAU, anawaomba wadau na serikali kukifahaumu kinachoendelea visiwani na kushiriki kukipatia tiba....

**SWALI: Ni unyanyasaji upi kwa wanawake unaouzungumzia?**

**JIBU:** Upo wa kimila japo unaelekea kukomeshwa unaohusu kutakasa wajane, wakilazimika kujamiiana ili kusafishwa au kuwatakasa watakapoolewa tena.

Wanalazimishwa kushiriki tendo la ndoa baada ya kufiwa. Yupo mwanaume aliyeandaliwa na anayefahamika kwenye jamii kuwa ni mahsusi kwa kazi hiyo. Licha ya kusababisha UKIMWI na VVU, magonjwa ya ngono, ni jambo linaoondoa heshima ya mwanamke kwa sababu kila mtu anafahamu kuwa ukifiwa utafanyiwa utakaso. Kuanzia watoto na jamii nzima na siyo siri.

Japo nyakati hizi matendo hayo yanatoweka, kuna visa vingine vya ukatili ambavyo ni matokeo ya athari za mabadiliko ya tabianchi kama kutelekeza wenza na watoto, rushwa ya ngono kwa watoto na wanawake, mimba za utotoni, ajira za wanawake bila malipo na hata za watoto pia.

**SWALI: Mnafanya kazi katika visiwa vipi?**

**JIBU:** Tuko Ukerewe Ukara , Goziba na Nansio ambavyo vutokana na mabadiliko ya tabianchi, rasilimali nyingi zimepungua hasa samaki, dagaa, misitu na kusababisha uhaba wa nishati jikoni na kusababisha matatizo mengi kwa mama na binti.

**SWALI: Nini hasa kinachotokea?**

**JIBU:** Uhaba wa samaki ziwani kutokana na kuvua kupindukia na kuharibika kwa ardhi ya kilimo kunawalazimisha wenyeji kuhama kutoka kisiwa kimoja kwenda kingine kusaka maisha hasa kuvua dagaa, kuwachambua na kuwabeba.

**SWALI: Kunaletaje ukatili na unyanyasaji?**

**JIBU:** Wanaume ndiyo wavuvi pia wanaohama kutoka kisiwa kimoja kwenda kingine na kuwaacha nyuma wanawake na watoto, wakati mwingine wazazi wote huondoka hapo watoto wanalazimika kujilea wenyewe, kufanya kaza ili kujikimu. Aidha, wanapoachwa wanakosa huduma zote kama chakula, elimu na mavazi. Kuna wengine wanaweza kutumbukia katika ngono, kupata mimba, maradhi, utoro shuleni, baadhi wanaolewa, wengine huondoka na kutumikishwa kwenye ajira ya watoto mikoani na visiwani kuosha, kuchambua na kuanika dagaa.

Pale wanapotelekezwa wakifika kwenye kambi za wavuvi pamoja na kusafisha dagaa, wanatumikishwa mfano kuuza pombe na sigara vilabuni na huwa mwanzo wa kusafirishwa kutumikishwa majumbani mikoani Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

**SWALI: Wanaume wanapokimbia na kutelekeza wenza na watoto wanakwenda wapi na kufanya nini?**

**JIBU:** Wanatoka kisiwa kimoja kwenda kingine kutafuta maisha, kisiwani wanapohamia kazi kubwa ni uvuvi wa dagaa, wakifanyakazi kwenye makambi ya wavuvi. Wanapoondoka watoto wao wanakwama kusoma, wanapata udumavu na unyafuzi kwa sababu ya lishe duni lakini na uvunjifu wa haki nyingi za mtoto kuanzia elimu na ulinzi.

Kinamama nao wanakwenda kwenye makambi ya uvuvi kuomba kazi, huko nako wananyanyaswa. Tunapata malalamiko kuwa ili kupata kazi ni lazima watoe rushwa ya ngono, pia kumlipa mwangilizi au 'supavaiza' 20,000 ili kupata nafasi, lakini lazima pia kupata bwana kwenye kambi ya uvuvi..

**SWALI: Wanawake wanafanya kazi gani kwenye kambi za uvuvi wa dagaa?**

**JIBU:** Kubwa ni kuwapikia na kuwahudumia wavuvi kambini



Sofia akifundisha wanawake (hawapo pichani). **PICHA: SAWAU**

na ili upate kazi utadaiwa ulipie 20,000 au utoe rushwa ya ngono, lakini ni lazima uchague mpenzi. Wanakulazimisha umchague unayempenda. Kama unaona aibu wanakuletea shuka utakalolipenda, hapo mwanaume anayelimiliki atajitambulisha na utakuwa umemchagua.

Lakini ukikataa umekosa kazi, kwa umoja wao watasema ni mwizi, unaiba vyakula vinapungua, watakusingizia uchawi wakitoa ushahidi, watadai una tabia mbaya na mengine ambayo yatasababisha ufukuzwe na mkuu au mmiliki wa kambi ya uvuvi.

Kwenye kambi za wavuvi mkuu wa kambi ndiye anayenunua vyakula na mwanamama anayeomba kazi jukumu lake ni kuvipika na kuwaandalia wavuvi na ndiyo wanaomlipa kwa vile nao mwajiri wao huwalipa kutokana na kazi wanayofanya kila siku.

Mwenye kambi huyo ndiye mwenye wavuvi, mitumbwi, boti na nyavu.

Katika hili kuna ukatili kwenye malipo, wavuvi hula na kukataa kumlipa mpishi hasa wakati wa mbalamwezi ambako dagaa wanaona mwanga ndani ya maji na kukimbia hivyo mavuno kuwa hafifu.

Kwenye giza dagaa wanapanda juu kufuata mwanga wa taa za wavuvi, kasha hunaswa kwa wingi, kipindi hicho mpishi analipwa hadi Shilingi 50,000 kwa mwezi lakini kwenye mbalamwezi dagaa hawajitokezi kwa wingi kama wakati wa giza na kusababisha mpishi kukosa ujira. Anaweza kukaa muda wote asilipwe na akakosa hela licha ya kuwapikia chakula na mwajiri wao kuwalipa, wavuvi hufanya wanavyotaka.

**SWALI: SAWAU inashughulikiaje tatizo hilo?**

**JIBU:** Tunafanyakazi na Mfuko wa Wanawake (WFT-T) kwenye miradi ya (uhimilivu) au kukabili mabadiliko ya tabianchi kwanza kwa kuieleza jamii kinachoyasababisha na kuhimiza uhimilivu.

**SWALI: Athari za mabadiliko hayo ni zipo huko Ukerewe?**

**JIBU:** Upungufu mkubwa wa dagaa na samaki visiwani, mazao hasa mihogo hakuna, ardhi imeharibika imejaa tindikali. Kwa kushirikiana WFT-T tunawahamasisha wanawake kulima viazi lishe. Tunahimiza kulima mazao ya muda mfupi lakini yenye kuhimili ukame, Ukerewe ni maarufu kwa mihogo lakini sasa haipatikani, imepungua wanategemea inayotoka Geita na Simiyu.

Samaki nao wamepungua kuanzia dagaa hadi sato na sangara, zamani watu walinunua samaki walivyotaka, waliwatumia kubadilishana na wengine ili kupata bidhaa walizohitaji. Leo ni haba, tena huuzwa kwa kilo. Kuna wakati wanauza sato kilo 9,000 au sangara hufikia kilo 7,000 au 6,000. Dagaa wamekwisha wanaopatikana ni wadogo tena wachungu.

Hata nao ni ghali hupatikana kwa taabu. Kilimo cha ndizi kimeathirika. Uvuvi haulipi hakuna samaki pia uvuvi haramu umeathiri mazingira na mazao ya ziwani.

Kwa ujumla maisha yamebadilika na athari za mabadiliko ya tabianchi zimeongeza unyanyasaji wa kijinsia, magonjwa ya kujamiina, mimba zisizotakiwa, utoaji mimba kiholela. Kuna uhaba wa nishati ya kupikia visiwani miti imekatwa mkaa na kuni havipatikani kwa unafuu.

Wanawake wanalazimika kutembea umbali mrefu kusaka kuni ni baada ya miti kukatwa sana .

Women Fund inaiwezesha SAWAU tangu mwaka juzi, kuwaelimsha wanawake na watoto jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kujiepusha na unyanyasaji kujua visababishi na kuepuka.

Tumewafikia wanawake zaidi ya1,000 na tunalenga kuleta mabadiliko na uhimilivu ikiwa ni pamoja na uwezeshaji kiuchumi kama kufuga dagaa, kuweka mikakati na kufanya uchechemuzi wa kupata nishati mbadala ya kupikia kama mkaa mbadala ili kuachana na kuni na mkaa , kutumia majiko banifu na nishati safi jikoni kama mkaa unaotokana na vumbi randa au taka za mazao.

Kwenye kilimo cha kisasa cha mboga na maboga badala ya kinamama kutegemea makambi ya wavuvi kufanyakazi za kupikia wavuvi, kubeba, kuchambua na kuweka madaraja ya dagaa lakini wakinyanyaswa na kudharauliwa utu wao.





## Wanasiasa kikwazo uhifadhi mazingira

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amesema viongozi hasa wa kisiasa wamekuwa kikwazo katika kukabiliana na suala la uchafuzi wa mazingira unaofanywa na baadhi ya watu wanaotupa taka ovyo mijini.

Alisema viongozi hao wamekuwa wakiwakumbatia na kuwakingia kifua watu hao hasa wanaochafua mitaro ya barabarani wasichukuliwe hatua na halmashauri kwa kigezo cha kulinda kura.

Serukamba alisema hayo juzi kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa baada ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Singida, Eliya Digha, kueleza kuwa kumekuwa na kasi ya baadhi ya wananchi kutupa taka barabarani na kushauri kuwekwe sheria kali za kuwachukukua hatua wahusika.

"Miji yetu hususani Manispaa ya Singida sio misafi lakini wanaoturudisha nyuma ni sisi viongozi tena wa kisiasa, unakwenda kufanyakazi ya kuwachukulia hatua wanaofanya uchafu anasema hapana usiwaguse," alisema.

Serukamba alisema katika kukabiliana na tatizo hilo halmashauri zinapaswa kuweka sheria kali za kudhibiti uchafu kama ilivyo katika Manispaa ya Moshi ambayo imefaulu kwa kuwatoza faini Sh.50,000 wanaobainika kuchafua mazingira.

"Tunajali sana wananchi wetu lakini hatujali maagizo, hii tabia lazima tubadilishe, hizi mvua zinazonyesha mitaro yote ikiziba maji yatajaa kwenye nyumba zetu na hawa ambao tunawatetea kwamba wasiguswe wakiingia kwenye maji watatulaumu na kusema serikali hii mipango yake mibaya," alisema.

Alizishauri halmashauri zote kutengeneza sheria ndogo kali ili mtu akikamatwa anatupa uchafu kwenye mitaro ya barabara au sehemu yeyote isiyostahili achukuliwe hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine.

"Kama mtu hapendi kupeleka taka kwenye dampo azihifadhi chumbani kwake sisi hatutamkamata, kwanini chumbani kwako huwezi kuweka taka lakini kwenye mitaro unatupa taka," alisema.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema katika kupendezesha miji yetu suala la upandaji miti lipewe kipaumbele hususani pembezoni mwa barabara.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Singida, Ibrahimu Kibasa, alisema katika mwaka huu wa fedha 2024/25 wakala huo umetengewa Sh. bilioni 22 katika utekelezaji miradi ya barabara mkoani hapa.

# Wasioandikisha watoto shule za awali kushtakiwa

**Na Paul Mabeja,** BAHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma imewaelekeza wazazi wenye watoto wa umri wa kuandikishwa kuanza shule, kufanya hivyo na atakayekaidi agizo hilo atapelekwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Ofisa Tarafa ya Bahi, Bahati Chai kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe, wakati wa sherehe za maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Mtoto iliyoandaliwa na Kanisa la Evangelistc Assemblies of God Tanzania (EAGT) Bahi.

Chai alisema wakati mwaka wa masomo kwa shule za msingi na sekondari nchini ukitarajiwa kuanza Januari 8, 2024, wazazi wote wenye watoto wenye sifa za kujiunga na masomo hawana budi kufanya hivyo bila kushurutishwa.

"Kuelekea mwaka ujao wa masomo na hivi sasa uandikishaji wa watoto kujiunga na darasa la kwanza unaendelea hivyo maagizo ya serikali ni wazazi wote kuhakikisha wanaandikisha watoto wao shule kabla hatujaanza kutumia nguvu," alisema Chai.

Alisema kwa mzazi yeyote ambaye atabainika kutomwandikisha shule mtoto ambaye anastahili atachukuliwa hatua kali ikiwamo kufikisha mahakamani.

"Kwa mujibu wa sheria kutomwandikisha shule mtoto ni sawa na kumfanyia ukatili wa kijinsia, hivyo wazazi wote wakati huu lazima mwandikishe shule watoto wenu kwani serikali tayari imefanya jukumu lake la kujenga shule na kuongeza madarasa," alisisitiza.

Aidha, alisema wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo la utoro wa wanafunzi shule pamoja na utumikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule kwenye uvuvi na kilimo.

"Bahi moja kati ya changamoto yake kubwa ni utoro kwa wanafunzi, lakini watoto wenye umri wa kwenda shule wanatumikishwa kwenye vibarua mbalimbali ikiwamo kwenye mabwawa ya uvuvi wa samaki.

"Hivyo, wakati mwaka wa masomo utakapoanza tusingependa kuona mtoto yeyote anaonekana katika maeneo ya kupala samaki au shambani kufanya vibarua badala ya kwenda shule," alisema.

Pia alisema ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini watoto wanapaswa kuwasikiliza wazazi wao badala ya mitandao ya kijamii ambayo imekuwa chanzo kikuu cha hali hiyo.

Naye Mchungaji wa Kanisa la EAGT Bahi, Jocktan Samwel, alisema kuna haja ya kuongeza kasi ya kuhubiri neno la Mungu kwa wazazi na watoto ili kukabiliana na changamoto ya mmomonyoko wa maadili.

Aliwakumbusha kusimamia watoto wao ili wapate haki yao ya msingi ya elimu na kupunguza idadi ya watoto wasiostaarabika jambo linalochangia kumomonyoka kwa maadili.

"Hata maandiko matakatifu yanaeleza kuwa usimwache elimu aende zake. Hii inamaanisha kuwa elimu ndiyo kila kitu watoto wetu hawawezi kupiga hatua katika maisha yao kama hawana elimu hivyo lazima tuiunge mkono serikali yetu ambayo imewekeza katika ujenzi wa shule na madarasa kwa kupeleka watoto wetu shule," alisema mchungaji Samwel.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza, Tanga, wakiwa katika harakati za kununua nguo za sikukuu jana katika soko la Jumatatu lililoko Mtaa wa Muheza Mjini. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# BRAC yatoa msaada vifaa vya mil. 303.7/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania (BMT) limetoa msaada wa vyerehani, vifaa vya saluni, kuku, ng'ombe, mbuzi na vifaa vya umwagiliaji kwa wajasiriamali 902 wa wilaya za Manyoni na Singida vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 303.7 ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Meneja wa Mkoa wa shirika hilo, Isihaka Mirambo, alisema vitu hivyo vimetolewa na shirika kupitia mradi wake wa kuwawezesha wanawake na mabinti balehe kiuchumi (AIM) baada ya wanawake hao kupewa mafunzo ya stadi za maisha ambayo walisajiliwa washiriki 2,400, lakini walioshiriki hadi mwisho ni 902.

Alitoa mchanganuo kuwa vyerehani watapewa wajasiriamali 226, seti za saluni watu 70, kuku 175 ambayo kila mmoja atapewa kuku 10 na dawa, ng'ombe 50, mbuzi watapatiwa watu 85 kwa kika mmoja mbuzi watatu na vifaa vya kilimo cha umwagiliaji watapewa wanawake 35.

Alisema wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wapatao 180 wamenufaika kwa kupewa vifaa vya shule ambavyo ni mabegi, madaftari, kalamu, penseli na sare za shule.

Mirwmbo alisema shirika hilo limetoa msaada huo kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha maisha ya wananchi kwa kugusa maeneo ambayo serikali haijayafikia ili kuwainua wananchi kiuchumi.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo na kuwa utasaidia kuondoa umaskini kwa wananchi hususani wanawake wa mkoani humo.

"Kupitia mradi huu wanawake mnakwenda kuwasaidia kinababa majukumu ya kifamilia kwasababu una salon yako unaweza ukawa unaingiza hata Sh. 20,000 kwa siku, ila usizitumie zote unaweka akiba zitakusaidia baadaye hata baba akikimbia wewe huna presha," alisema.

Dk. Mganga alisema ni jukumu la kila mwanamke aliyepewa vitu hivyo kujitambua, kujituma, kujitoa, kuvitumia na kujiwekea akiba ili viweze kuleta matokeo chanya.

"Leo tunapewa vifaa hivi sitegemei vifaa vinakwenda kukaa mwezi mzima nyumbani kama mapambo nina imani kila mtu atatafuta sehemu nzuri ya kufanyia shughuli zake, hatutegemei mtu aje na hadithi kwamba ameibiwa na atakayefanya uzembe vikaibiwa tutamchukulia hatua," alisema.

Aliongeza kuwa ni marufuku kwa mwanamke yeyote aliyepewa vifaa hivyo kuviuza na kuwaagiza maofisa maendeleo kuwafuatilia wanufaika wote kujua kama wanaendelea kuvitumia na kuwasaidia kutafuta wateja badala ya kuwaacha tu kama picha.

Alishauri kila mnufaika aweke mpango kazi wake wa biashara kwa kutumia elimu ya ujasiriamali waliyofundishwa na kuonya wanawake watakapoanza kupata pesa wasizitelekeze familia zao.

"Baadhi ya wanawake wakishaboreka kiuchumi tunaanza kuleta dharau katika familia, huu mradi tuliopewa sio kwenda kuvunja familia, busara na hekima ni pale unaimarika kiuchumi na kuendelea kumheshimu mume wako na kutunza familia yako," alisema.





# Mpokwa ataja sababu CCM kuwa tegemezi Rungwe

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Rungwe, Abdalah Mpokwa, amesema chama hicho hakina mradi wowote katika wilaya hiyo ambao unakiingizia kipato hali inayokifanya kuwa tegemezi na kushindwa kutekeleza kwa wakati baadhi ya majukumu yake.

Mpokwa aliyasema hayo juzi kwenye mkutano maalumu wa chama hicho wa kumpokea Mwenyekiti wa Chama hicho Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge ambaye anaendelea na ziara kwenye wilaya za mkoa huo kwa ajili ya kujitambulisha.

Alisema kutokana na hali hiyo wameandaa mpango wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo itakuwa inakiingizia chama hicho fedha kwa ajili ya uendeshaji badala ya kutegemea misaada na michango ya wadau pekee.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ukumbi wa mikutano wa kukodisha, vibanda vya biashara ambayo yote itakuwa Tukuyu Mjini mahali zilipo ofisi za chama na mashine kuchakata kahawa.

"Kuna wakati kama chama huwa tunakwama kutekeleza baadhi ya majukumu lakini tunakwama kutokana na ukata, kwa hiyo tumekuja na mikakati hii ili tujikwamue kiuchumi," alisema Mpokwa.

Kuhusu uhai wa chama katika wilaya hiyo, Mpokwa alisema chama hicho kina idadi kubwa ya wanachama ambao wanakipa uhakika wa kushinda kwenye chaguzi mbalimbali.

Alisema kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2019 na uchaguzi mkuu wa 2020 chama hicho kilishinda kwa asilimia kubwa kwenye nafasi zote ambazo zilikuwa zinawaniwa ikiwamo kushinda majimbo yote mawili ya wilaya hiyo.

Mwalunenge alisema atakaa na viongozi wa chama hicho katika wilaya zote za mkoa huo ili kutathmini miradi yote ambayo wanakusudia kuitekeleza na kuangalia namna ya kuikamilisha.


Alisema anaendelea na ziara katika wilaya zote kwa lengo la kujitambulisha na ataitumia mikutano yake hiyo kusaidiana na viongozi wa chama hicho kuibua miradi na kujadili namna ya kuitekeleza.

Aliwashukuru wanachama wa chama hicho katika Mkoa wa Mbeya kwa kuendelea kukiunga mkono na kushirikiana kukijenga pamoja na kuendelea kuwachagua wagombea wa chama hicho kwenye kila uchaguzi wa serikali.

"Nakusudia kujenga hospitali katika wilaya hii ya Rungwe ili kuwasaidia wananchi wenzangu lakini pia tutaendelea kushirikiana kwenye miradi mbalimbali ambayo mtakuwa mnaiibua ili tuikamilishe na ianze kutuhudumia," alisema Mwalunenge.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, aliwaomba wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuwapatia ushirikiano viongozi wa chama hicho ili waendelee kuwatumikia.

Alisema serikali imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Mbeya ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya, maji na barabara na hivyo akawataka wananchi kuendelea kushirikiana na serikali yao kutekeleza miradi hiyo.



Meneja Rasilimali Watu wa Vodacom Tanzania PLC, Naiman Moshi (kulia), akikabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo ya TEHAMA na sayansi kwa mwanafunzi aliyehitimu kidato cha nne Shule ya Sekondari ya Samoja, Sarafina Mussa Sanga, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. Kupitia programu inayojulikana kama 'Code Like a Girl' kwa kushirikiana na Tanzania Data Lab (dLab), imefanikisha mafunzo ya TEHAMA na Coding kwa zaidi ya wanafunzi wa kike 1,750 pamoja na kuwapa ushauri wa kitaaluma ili kuwajenga kimasomo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waishukuru serikali kukamilisha mradi wa majisafi Wanging'ombe

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

WANUFAIKA wa mradi wa Igando-Kijombe Wilaya ya Wanging'ombe Mkoa wa Njombe, wameishukuru serikali kwa kukamilisha mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 12 na kuwaondoa kwenye adha ya kutumia maji pamoja na mifugo ikiwamo ng'ombe.

Wakizungumza mbele ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani, wananchi hao walisema hapo awali walikuwa wakifuata maji umbali mrefu.

Andokise Kaboi ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Malangali alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kuwaepusha na magonjwa ya matumbo na kuhara kutokana na matumizi ya maji yasiyo salama.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kukamilisha mradi huu, tangu uhuru hatujawahi kupata maji, tunamshukuru sana Rais Samia kwa hivi sasa hatutaumwa tena matumbo, alisema Kaboi.

Naye Shukulu Mwalila alisema kuwa changamoto ya upatikanaji wa maji katika vijiji vyao ilikuwa ni kubwa hali iliyokuwa inasababisha kutumia maji pamoja na mifugo.

"Tunaenda kuchota maji lakini ukifika kule unakuta ng'ombe wanakunywa, wanachafua kwa hiyo sisi kuumwa magonjwa kama ya tumbo ilikuwa ni kawaida," alisema Mwalila.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa Wakala ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Wanging'ombe, Mhandisi Josh Chum, alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 95 na tayari umeanza kutoa maji katika Kijiji cha Malangali.

Chum alisema kuwa Mradi wa maji Igando-Kijombe ni mradi uliosanifiwa kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama na utakapokamilika utahudumia vijiji 10 na jumla ya wakazi wapatao 14,377 watanufaika.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Julias Peter, alipongeza jitihada za serikali katika kufikisha majisafi na salama kwa wananchi kama Ilani ya uchaguzi ilivyoelekeza..

# Tulia Trust yatimiza ndoto ya mwanafunzi Ester

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

TAASISI ya Tulia Trust imemkabidhi kiti mwendo mtoto, Esther Seme (8) mkazi wa Kijiji cha Ilolo, Kata ya Kiwira, Wilaya ya Rungwe katika Mkoa wa Mbeya ambaye ni mlemavu wa viungo kwa ajili ya kumsaidia kwenda shuleni.

Kiti hicho kilikabidhiwa kwenye familia ya binti huyo na Ofisa Habari wa Taasisi hiyo, Joshua Mwakanolo wakati wa mbio maalumu za bendera zilizoanzisha na taasisi hiyo kwa ajili ya kuwasaidia watu mbalimbali wenye mahitaji.

Mwakanolo alisema waliamua kumsaidia binti huyo kutokana na kupokea maombi maalumu kutoka kwenye familia hiyo ambayo imekuwa ikipata shida namna ya kumsaidia.

Alisema wakati wa kuanza kwa mbio hizo za bendera waliwatambua watu wote ambao wana mahitaji ili waanze michakato ya kuwasaidia na kwamba mbio hizo za bendera zinatumika pia kuitambulisha taasisi hiyo.

"Wapo maofisa wetu kwenye maeneo yote ambao kazi yao ni kupokea maombi ya wenye mahitaji na kuhakiki, sasa mbio hizi mbali na kumsaidia binti huyu pia tutawasaidia wazee na watu wengine wenye mahitaji hasa wenye ulemavu," alisema Mwakanolo.

Akipokea bendera kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Ally Kiumwa, alipongeza Taasisi ya Tulia Trust kwa kuwakumbuka watu wenye mahitaji maalumu.

Alisema misaada ambayo inatolewa na taasisi hiyo ni sadaka ambayo lazima ikimbukwe na watu wanaonufaika nayo na hivyo akawataka wananchi wote walionufaika kuitumia vizuri misaada hiyo.

Alisema serikali kwa sasa imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha inahudumia makundi maalumu ikiwamo kuanzisha sera ya elimu jumuishi pamoja na matibabu bure kwa wazee.

**Alisema wakati wa kuanza kwa mbio hizo za bendera waliwatambua watu wote ambao wana mahitaji ili waanze michakato ya kuwasaidia na kwamba mbio hizo za bendera zinatumika pia kuitambulisha taasisi hiyo.**



## Serikali yajizatiti kukamilisha ujenzi wa barabara vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema azma yake katika kipindi cha miaka miwili 2023-2024 ni kukamilisha ujenzi wa barabara zote za vijijini zenye urefu wa kilomita 250 ikiwamo zile zinazokwenda katika miradi ya hoteli za kitalii na maeneo ya uwekezaji.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati alipozungumza na wananchi na mkandarasi kampuni ya Orkun anayejenga barabara ya Charawe, Ukongoroni yenye urefu wa kilomita sita ambayo ni ahadi ya Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili barabara zote za vijijini ikiwamo zile ambazo hazijawahi kutiwa lami zimeorodheshwa kwa ajili ya ujenzi wake kwa kiwango cha lami.

Alisema barabara ya Ukongoroni ambayo ilikuwapo kabla ya mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 haijatiwa lami badala yake ujenzi wake ulikuwa ukifanyika kwa njia ya kupara na kutia kifusi.

"Ujenzi wa barabara ya Ukongoroni hadi Charawe ni ahadi ya Rais, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuona kwamba barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami hatua ambayo itarahisisha huduma za maendeleo ikiwamo sekta ya kilimo," alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea na ujenzi wa barabara zote za ndani zinazokwenda katika miradi ya sekta ya utalii ikiwamo katika kijiji cha Nungwi chenye idadi kubwa ya hoteli.

Alisema kwa muda mrefu yamekuwapo malalamiko ya wawekezaji kuhusu ubovu wa barabara ambazo nyingine haziwezi kufikika katika hoteli za kitalii ambapo kwa kawaida jukumu la ujenzi wa barabara ni la serikali.

"Tumekisikia kilio cha wamiliki wa hoteli za kitalii zilioko Unguja na Pemba na sasa tumeanza ujenzi wa barabara za ndani zinazokwenda katika miradi ya utalii kwa kuanzia kijiji cha Nungwi,"alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Shomari Omar Shomari, alisema kasi ya ujenzi wa barabara za ndani zinazokwenda katika miradi ya utalii ni kubwa kwa kuanzia katika kijiji cha Nungwi.

Aidha alisema barabara kuu inayokwenda katika kijiji cha Nungwi kutoka mjini itafanyiwa marekebisho baadhi ya maeneo ili kupitika vizuri kufuatia kuharibika katika kipindi cha mvua zinazoendelea kunyesha. "Tunaendelea na kasi ya ujenzi wa barabara za ndani zinazokwenda katika miradi ya utalii katika kijiji cha Nungwi ambapo matarajio yetu tukimaliza tutakwenda maeneo mengine ikiwamo Kiwengwa," alisema.

Ujenzi kama huo wa barabara za vijijini pamoja na maeneo ya uwekezaji unafanyika pia katika kisiwa cha Pemba kwa ajili ya kuvutia wawekezaji.

# ACT yaonya masheha kuvuruga amani Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo Zanzibar kimesema kama masheha wataendelea kuwabagua wananchi katika kutoa barua za kuwawezesha kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (ZAN ID), watasababisha machafuko na kuvuruga amani na umoja wa kitaifa.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika katika Jimbo la Pangawe Wilaya ya Magharib B Unguja.

Duni alisema tangu zoezi la uandikishaji la wapigakura wa kudumu kuanza kufanyika kuna watu wengi wamekwama kuandikishwa baada ya kukosa barua za kuthibitishwa na masheha jambo ambalo limewanyima haki ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ambacho ndio hutumika katika uandikishaji wa wapigakura.

"Sheha anashindwa kufahamu kwamba anafanya dhambi zitakazowarithisha wajukuu zetu, moja kati ya tatizo kubwa huko tunakokwenda na suala la uraia Wazanzibari tutakuwa wachache kuliko wageni tutateswa kuliko Palestina, haikuanza juzi kule Palestina ilianza kidogo kidogo suala la ubaguzi Zanzibar ni maafa," alisema Duni.

Alisema tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi masheha wamekuwa ni kikwazo kwa wananchi kupata haki ya uraia na kuwakosesha haki ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa jambo ambalo halikubiliki katika misingi ya demokrasia na utawala bora.

Mwenyekiti huyo alisema hali inayojitokeza Zanzibar haikubaliki na kuwataka wanachama wa chama hicho wanaponyimwa barua na masheha wasikubali na badala yake waendelee kudai kwa sababu ni haki yao.

Alisema mbali na tatizo hilo kumeibuka tatizo la watu kukwama kuandikishwa kutokana na mashine inayotumia alama ya kidole kutosomeka katika mfumo wa daftari la uandikishwaji na tatizo hilo kuwaathiri zaidi wapinzani.

Alisema Tume ya Uchaguzi inafanya hivyo kwa makusudi kwa dhumuni la kuibeba CCM kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025, lakini ACT hakitokubali kufanyiwa mizengwe katika uchaguzi huo.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Nassor Ahmed Mazrui, alisema matatizo yanayoendelea kujitokeza katika suala hilo hayapaswi kuwapo ili kudumisha amani na kujenga msingi ya umoja wa kitaifa.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema mfumuko wa bei za bidhaa uliojitokeza Zanzibar umesababishwa na serikali kubinafsisha huduma za uendeshi wa Bandari ya Malindi kwa kampuni moja kutoka Ufaransa.

"Wawekezaji hawa hakuna walichowekeza tangu wakabidhiwe bandari wanatumia kalamu na karatasi za Shirika la Bandari lakini kazi yao kubwa kuongeza na kuanzisha tozo mpya jambo ambalo limesababisha mfumuko wa bei," alisema. Alisema kuna wafanyabiashara wenye asili ya India wamehamisha bidhaa zao Zanzibar kutokana na kupanda kwa tozo za usafirishaji wa mizigo na mazingira magumu ya biashara tangu wawekezaji hao kukabidhiwa Bandari ya Malindi.

Aidha, alishangazwa na ukarabati wa Uwanja wa Amani wenye uwezo wa kuchukua watu 16,000 kugharimu karibu Sh. bilioni 52 wakati uwanja kiasi kikubwa zaidi ya gharama za ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ya Sh. bilioni 32 unaochukua watu 60,000.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alisema matatizo yanayojitokeza Zanzibar yanatokana na kutokuwa na mamlaka kamili na kuwanyima haki wananchi ya kuchagua viongozi wanaowataka.



Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, akisalimiana na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, alipowasili katika mkutano wa hadhara wa chama hicho Jimbo la Pangawe, Mkoa wa Mjini Magharib Unguja. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Marekebisho ya Sheria ya ZIPA kufungua mlango wa uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAREKEBISHO ya Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji (ZIPA) yaliyopitishwa hivi karibuni na Baraza la Wawakilishi yatafungua milango zaidi kwa wawekezaji kuwekeza Zanzibar huku mchakato wa uwekezaji ukikamilika katika kipindi kifupi na kuondosha urasimu.

Mwekezaji wa Kisiwa cha Changuu na Bawe, Andrea Davide Azzola, akizungumza na waandishi wa habari jana visiwani humo, alisema amefurahishwa na marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi ZIPA ambayo yanamwezesha mwekezaji kukamilisha mambo yote ya msingi ikiwamo kupata kibali cha ardhi bila ya urasimu.

Alisema sheria iliyokuwapo awali ilikuwa na upungufu mwingi ambao si rafiki kwa mwekezaji kuwekeza katika kipindi kifupi na kuanza kutekeleza mradi wake katika eneo la kupata ardhi.

Azzola mwenye kampuni ya "Cocoon Collection" ni miongoni mwa wawekezaji wakubwa Zanzibar waliowekeza mtaji wa dola za kimarekani milioni 25 ikiwamo uwekezaji katika kisiwa cha Changuu na Bawe pamoja na Hoteli ya Kendwa iliopo Nungwi na Pongwe visiwani humo.

Alisema miradi hiyo imetoa jumla ya ajira 1,100 kati ya hizo 1,050 ni wazawa sawa na asilimia 95 huku wakulima wa wavuvi wakipata nafasi kubwa ya kuuza bidhaa zao katika hoteli hizo.

"Nimefurahishwa na sheria mpya ya uwekezaji ya Zanzibar ambayo imeondoa urasimu na kutufanya sisi wawekezaji kukamilisha mambo yetu ikiwamo kupata kibali katika kipindi kifupi sana," alisema.

Naye Mwekezaji wa Hoteli ya Marumbi Blue Bay, Erich Fiescher, alisema Sheria ya Mamlaka ya Vitega Uchumi ya Zanzibar ni nzuri ambayo imelenga katika kuwavutia wawekezaji kwa kuonesha mahitaji yaliopo sasa.

Alisema kitendo cha kuifanya Mamlaka ya Uwekezaji ZIPA kuwa kituo kimoja cha uwekezaji ni hatua moja muhimu ambayo itawavutia wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwamo ya kimkakati.

"Nimefurahishwa na Sheria mpya ya Mamlaka ya Vitega Uchumi ZIPA ambayo imekuja wakati mwafaka wa mahitaji yaliopo sasa yanayokwenda na wakati ikiwamo kuingiza uchumi wa buluu na uwekezaji wake ambapo awali yalikuwa hayapo kisheria," alisema.

Mwekezaji mzalendo anayejishughulisha na ufugaji wa wanyama Wilaya ya Magharibi Unguja, Jumbe Ismaili Ali, alisema sheria hiyo imekuja kumlinda na kumwezesha mwekezaji mzalendo na yeye kufaidika na fursa za uwekezaji ikiwamo misamaha ya kodi.

"Ni sheria nzuri ambayo sasa itatuwezesha sisi wawekezaji wazalendo kuwekeza katika shughuli zetu za uwekezaji kama walivyokuwa wageni," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisema marekebisho ya sheria hiyo ni matokeo ya maono ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika safari ya uwekezaji wenye tija unaokwenda na wakati.

"Sheria iliyopitishwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi inakwenda na wakati wa mahitaji yaliopo sasa ambayo imetoa fursa kwa wawekezaji wazalendo katika uwekezaji huku miradi ya uchumi wa buluu ikijumuishwa," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MUSA JILUGU DAUD** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0883-0142** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DON BOSCO-DIDIA SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/2099/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CHOMBO HAMISI SIMBA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 352 ADD.** Kwa yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu.

Taarifa Polisi:

**PHQ/TAN/3294/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MUSA SAIDI MWIDADI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 166 CDL** aina ya **HONDA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DAR/KIN/55952/2023.**

---

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB NA: CDA/ED/LA-15/25981**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: MERABU OTHINIEL**
**ARDHI: KIWANJA NA. 109 KITALU ' A' ENEO LA MAPINDUZI NORTH**
**MWOMBAJI: MERABU OTHINIEL**

TAARIFA IMETOLEWA, kwamba Barua ya Toleo iliyotajwa hao juu imepotea na ninakusudia kutoa hati Milki mpya badala yake iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa siku thelathini (30) tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

BARUA YA TOLEO NAKALA HALISI ikionekana, irudishwe kwa:

Imetolewa na:
Adinani I. Omari
Afisa Ardhi Mteule
DODOMA,

15 Disemba, 2023.

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27577 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MEGHA KANAIVAL**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CHETAN VIDON BHATT**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above – named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23 day of 01, 2024.

**DATED** at **DAR ES SALAAM** this 14 day of 12 , 2023.

Senior Resident Magistrate

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya MASASI**
**Kituo Cha LISEKESE Mkoa MTWARA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na.72 /2023**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: AHAMADI HASSANI IBRAHIM – WA CHIKUNDI**
**K.K. AFISA MTENDAJI CHIKUNDI – MASASI**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**MADAI YA FEDHA TSH. 2,548,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 21 mwezi 12 mwaka 2023 saa 02:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa Kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 14 mwezi 12 mwaka 2023.

Hakimu

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo Cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 99/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JUMA JUMANNE BAKARI WA NKUHUNGU KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA RAMADHANI JUMANNE BAKARI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo Tarehe 14 Mwezi 12 Mwaka 2023**

................. .............

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTATION COUSE 27836 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE STEPHEN NZOGYA NZULLIGA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY MAGRETH JONATHAN LEONARD**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of the letters of administration is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filled on or before the 15 day of 1, 2024

Dated at Dodoma this 03rd day of October, 2023

PETITIONER

Dated at Dodoma this 13th day of December, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 97/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ROBERTADOTTO J. OWURE wa KIKUYU DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JOSEPHAZIZI KHALID NYONI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 08 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

***Zingatia;***

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 08 Mwezi 12 Mwaka 2023.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**
**SHAUIR LA MADAI Na. 225 YA 2023**
**RITHA MICHAEL CHUWA.............MDAI**
**DHIDI YA**
**1ST ELIBARIK MARCO TILLE**
**2ND NOVELISTIC NITRICIOUS COURT LIMITED................WADAIWA**

**Kwa: 1ST ELIBARIK MACRO TILLE – DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta madai yake ambayo yamesikilizwa na kufikiwa kupangiwa uamuzi, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya Wilaya binafsi au Wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa siku ya tarehe 21 Mwezi 12 Mwaka 2023 saa mbili (2:00) kamili asubuhi, kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja n a vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 18/12/2023.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......132/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JOSEPH MOSILLE wa K/NDEGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ANNA JOSEPH**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 12 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mahakama kutathmini sheria mapenzi jinsi moja Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

MAHAKAMA ya kikatiba nchini Uganda imepokea ushahidi uliowasilishwa na pande mbili katika kesi ya kupinga sheria dhidi ya mapenzi ya jinsi moja nchini humo.

Inaelezwa kuwa mahakama hiyo sasa itaangalia na kutathmini ushahidi wa kila upande na kutangaza tarehe ya kutoa hukumu.

Kesi ya kupinga sheria dhidi ya mapenzi ya jinsi moja iliwasilisha na watetezi wa haki za kibinadamu, asasi za kiraia pamoja na watu mbalimbali wakidai sheria hiyo inakiuka haki za kibinadamu.

Lakini upande wa utetezi ukiongozwa na mwanasheria mkuu wa serikali unasema sheria hiyo inalenga kulinda familia na maadili ya utamaduni wa nchi hiyo.

Sheria hiyo ilitiwa saini na Rais Yoweri Museveni, Mei 26, mwaka huu na hivyo kuwa sheria kamili. Huku moja ya vipengele vitatu katika sheria hiyo ikiwa ni adhabu ya kifungo cha maisha na adhabu ya kifo kwa wanaopatikana na hatia ya kufanya mapenzi ya jinsi moja nchini Uganda.

Hata hivyo tangu kupitishwa kwake, sheria hiyo imekuwa ikikosolewa vikali na nchi za magharibi.

Marekani tayari imewawekea vikwazo baadhi ya maofisa katika serikali ya Uganda kwa kutuhumiwa kuminya haki za kibindamu na nchi hiyo pia imeondolewa kutoka kwenye mpango maalumu wa kibiashara wa (AGOA).

Vile vile inaelezwa kuwa hiyo si mara ya kwanza mahakama ya kikatiba kusikiliza kesi kuhusu sheria dhidi ya mapenzi ya jinsi moja, na kwamba Agosti 2014, ilibatilisha sheria kupinga mapenzi hayo kwa misingi ya utaratibu kutokana na kura za wabunge kutotimia ili kuipitisha. **BBC**

# CENI: Tumejipanga vizuri uchaguzi wa kesho

**KINSHASA,** DRC

IKIWA imebaki siku moja uchaguzi mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ufanyike, serikali imetangaza kupokea ndege mbili za mizigo kutoka jeshi la Misri ili kusafirisha vifaa vya uchaguzi mashariki mwa nchi hiyo.

Awali Tume Huru ya Uchaguzi (CENI) ilieleza kuwa moja ya changamoto zinazowakabili ni ugumu uliopo katika kufikisha vifaa vya uchaguzi katika maeneo ya mashariki mwa nchi hiyo kutokana na tatizo la miundombinu ya barabara.

Baada ya hatua hiyo tume hiyo ilielezea utayari wake wa kufanyika uchaguzi kote nchini humo, huku ikieleza kuwa vifaa mbalimbali ikiwamo karatasi za kura na fomu za kuorodhesha matukio ya uchaguzi katika kila kituo cha kupigia kura vimeshawasili nchini humo na kusambazwa kwenye mikoa yote 29.

Msemaji wa tume hiyo, Patiricia Nseya alisema, "Nithibitishie kwamba kila kitu kinafanywa ili uchaguzi wa Desemba 20 ufanyike. Kuna vifaa vya uchaguzi kama vile mashine ya kupigia kura tayari vimetawanywa kote nchini.

"Tumepata ndege za mizigo na helikopta ambazo zimeendelea kupeleka vifaa vingine kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni moja ya jitihada za kutatua changamoto za usambazaji wa vifaa hivyo," alisema.

Pia tume hiyo ilisema katika Jimbo la Ituri huko Kaskazini Mashariki mwa DRC vifaa vya uchaguzi vimetawanywa kwa asilimia 99 kwa msaada wa ndege za kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa, Monusco.

Hata hivyo ilielezwa kuwa DGC ambayo haina miundombinu mizuri ya barabara inategemea kwa asilimia kubwa usafiri wa ndege. Na kwamba kumekuwa na wasiwasi kwamba vifaa vya uchaguzi huenda vikachelewa kufikishwa kwenye vituo 75,000 vya kupigia kura ifikapo kesho.

Wakati hayo yakiendelea, wagombea wa urais walihitimisha kampeni zao usiku wa jana, ambako Rais Felix Tshisekedi anayewania muhula wa pili, alihitimisha kampeni yake hapa Mjini Kinshasa kwa kuitisha mkutano wa hadhara.

Pia ilielezwa kuwa mpinzani wake Moise Katumbi ilihitimisha kampeni yake huko Kananga jimboni Kassai ambayo ndio ngome ya rais wa sasa.

Katika hatua nyingine duru za usalama nchini humo zilieleza kuwa kwa ujumla kampeni hizo zilizodumu siku 30 zilifanyika kwa utulivu licha ya vurugu chache zilizosababisha watu wawili kuuawa.

Wakati huohuo waangalizi wa uchaguzi kutoka Umoja wa Afrika waliwasili nchini humo, ikielezwa kuwa ujumbe wa watu 80 unatarajiwa kutawanywa katika maeneo kadhaa ya DRC.

Vile vile ilibainishwa kuwa waangalizi hao waliwasili nchini humo baada ya wale wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Kusini mwa Afrika, (SADC) na wa kituo cha Carter Center kutoka Marekani.

Kwa upande wa Umoja wa Ulaya uliondoa waangalizi wake baada ya serikali ya DRC kutoruhusu kuingizwa kwa baadhi ya vifaa vya mawasiliano vya ujumbe huo.

**DW**




Msemaji wa Tume ya Uchaguzi ya Kongo (CENI), Patricia Nseya. **PICHA: MTANDAO**

# Kenya yakataa kuwakamata wanasiasa wa DRC



**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya, William Ruto, amebainisha kukataa ombi la kukamatwa kwa wanasiasa wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) walioanzisha muungano na waasi mjini Nairobi Ijumaa.

Mkuu wa zamani wa Baraza la Uchaguzi la DRC, Corneille Nangaa, pamoja na kiongozi wa M23 Bertrand Bisimwa, siku chache zilizopita alitangaza akiwa Kenya kwamba anaunda muungano wa kisiasa na kijeshi na waasi wa M23 na makundi mengine yenye silaha kwa lengo la kurejesha amani.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo iliibua jibu la hasira kutoka kwa serikali ya DRC ambayo ilionya Kenya kuhusu matokeo ya kumkaribisha Nangaa.

Kutokana na hali hiyo, Rais Ruto alisema kuwa amekataa kutii ombi la kuwakamata wanasiasa hao wa DRC, akilitaja suala hilo kuwa sio la kidemokrasia.

"Kenya ni demokrasia. Hatuwezi kumkamata yeyote ambaye ametoa taarifa. Hatuwakamati watu kwa kutoa matamshi, tunawakamata wahalifu," alisema Rais Ruto.

Pia ilielezwa kuwa serikali ya Kongo ilimwita balozi wa Kenya mjini Kinshasa na pia kumrudisha nyumbani balozi wake wa Nairobi kwa mashauriano.

Rais Ruto alisema ni haki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kufanya hivyo, "Lakini siwezi kumkamata mtu yeyote kwa sababu tu walitoa taarifa. Hiyo ni kinyume cha demokrasia na sivyo Kenya ilivyo."

Wizara ya Mambo ya Nje ya Kenya hapo awali ilisema inajitenga vikali na masuala ya ndani ya DRC, na imeanza kuchunguza suala hilo.

**BBC**

# TPLB YATOA NENO VAR KUTUMIKA KWA MKAPA

Na Adam Fungamwango

BODI ya Ligi imeeleza kufurahishwa habari ya kutumika kwa Teknolojia ya Kumsaidia Mwamuzi (VAR) hapa nchini, ikikiri kuwa uamuzi wa kutegemea jicho la mwamuzi au wasaidizi wake wawili pekee umeshapitwa na wakati.

Ofisa Habari wa Bodi hiyo, Karim Boimanda, alisema hayo jana siku chache tu baada ya Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, kutangaza kupokea vifaa hivyo kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kwenye Mkutano Mkuu wa 18 wa Shirikisho hilo uliofanyika mkoani Iringa, ambapo vinatarajia kufungwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Boimanda alisema wao kama Bodi imekuwa kama sherehe na amewataka wapenzi wa michezo na wadau kuungana na kuunga mkono jambo hilo lililosubiriwa kwa muda mrefu badala ya kuzuka mjadala wa kwa nini VAR hiyo itatumika kwenye uwanja mmoja tu.

"Miaka mitatu sasa tumekuwa tukisema kuwa uamuzi ya kutegemea jicho la mwamuzi pekee umeshapitwa na wakati kwa sababu ufanisi wake ni mgumu sana kuupata kwa asilimia kubwa, sisi tunaendelea nao kwa sababu hatuna uwezo wa kuwa nazo, kwa hiyo taarifa za kuja kwa VAR kwetu ni kama sherehe hivi kwa sababu tunaona namna ambavyo tunaenda eneo ambalo tulikuwa tunalisubiri kwa hamu," alisema Boimanda.

Hata hivyo, kumekuwa na mijadala mbalimbali vijiweni, kwenye baadhi ya vyombo vya habari kuwa iwapo itakuwa kwenye uwanja mmoja tu, haitokuwa haki kwa michezo itakayochezwa kwenye viwanja vingine, kwani Benjamin Mkapa mechi itachezwa kwa umakini kwa sababu kuna VAR, lakini viwanja vingine kunakuwa na makosa na timu inanyimwa haki yake.

"Kama nilivyosema VAR gharama yake ni kubwa, ukitaka ije hapa kwa viwanja 10, au 12 ni changamoto kwa hiyo ni lazima kwanza sisi kama Watanzania, sasa hapa nazungumza kama Mtanzania, inabidi kwanza tupokee kwanza kama inakuja kwa uwanja mmoja, halafu baadaye tutapata nafasi ya kujadili vipi kuhusu viwanja vingine, ni sawa na mtu amejitokeza kukununulia chai ya asubuhi halafu kabla hujanywa unaanza kulalamika kwa mchana itakuwaje, gonga kwanza kifungua kinywa, halafu baadaye uanze kukomaa na chakula cha mchana, kwa sasa Watanzania tuombe dua jambo hili likamilike ili tuangalie hayo ya baadaye," alisema.

ACHENI WAJE...



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini, timu hiyo itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kesho kuikaribisha Medeama ya Ghana katika mchezo wa marudiano wa Kundi D Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: YANGA**

## JKT Queens yataka pointi 9 za ugenini

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, amesema mikakati yake ni kuona kikosi chake kinavuna alama tisa za ugenini katika michezo mitatu ya kwanza ya msimu wa 2023/24 wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

JKT Queens itaanza msimu kwa kucheza ugenini dhidi ya Bunda Queens kesho katika Uwanja wa Karume mkoani Mara baada ya hapo itavaana na Geita Gold Queens mchezo utakaopigwa Nyankumbu, kisha itaelekea mkoani Lindi kukabiliana na Amani Queens katika dimba la Ilulu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha huyo alisema baada ya mchezo wa fainali wa Ngao ya Jamii, wamefanyia kazi mapungufu yao na sasa kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kutafuta alama muhimu dhidi ya Bunda Queens.

**Alisema wamejiandaa vizurina kuhakikisha wanaanza vizuri kwa kukusanya alama muhimu katika michezo hiyo mitatu ambayo watakuwa ugenini.**

"Mipango yetu kwa msimu huu ni kukusanya pointi tatu katika kila mechi, tunacheza ugenini na tumejipanga vizuri kwa ajili ya kutetea taji letu na kuanza vizuri msimu kwa ushindi dhidi ya Bunda Queens," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema anaamini haitakuwa mechi rahisi kutokana na maboresho yaliyofanywa na timu msimu huu huku akiamini kuwa mchezo wao dhidi ya Bunda Queens utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa kikosi chao.

Alisema wanatakiwa kuwaheshimu wapinzani wao hao ili kuweza kupata matokeo mazuri na kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa sababu wako ugenini na wanapambana kutafuta pointi tatu mbele ya wenyeji wao ambao watakuwa na sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki wao.

# KVZ kutema sita, kusajili saba wapya

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAKATI dirisha dogo la usajili Ligi Kuu Zanzibar likiwa limefunguliwa mwishoni mwa wiki huku likitarajiwa kufungwa rasmi Januari 16, mwakani, timu ya KVZ FC imesema inakusudia kufanya usajili wa wachezaji saba katika kipindi hiki ili kukiongezea nguvu kikosi chao.

Wachezaji hao wanaotarajiwa kuongezwa katika kikosi hicho watano watatoka nje ya Zanzibar na wawili ni kutoka nje ya Tanzania, lengo likiwa ni kujiweka sawa kuelekea mzunguko wa lala salama na mbio zao za ubingwa wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Mohammed, alisema mbali na kusajili wapya saba, pia wataachana na wachezaji sita huku nafasi watakazozipa kipaumbele katika usajili huo ni ya ushambuliaji, ulinzi pamoja na mlinda mlango.

Alisema nafasi hizo ndio zilizompa wakati mgumu katika mzunguko huu wa kwanza, hivyo mpango wake ni kuhakikisha anaziba mapengo yote yaliyojitokeza.

Mohammed alisema anataka kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa na kupata kile kinachohitaji hasa katika malengo yao ya kuutaka ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

"Tupo makini katika kufanya mapendekezo ya kupata wachezaji wazuri, wenye uwezo na kiwango kikubwa cha kupambana katika mzunguko wa lala salama hasa kutimiza lengo letu la ubingwa, na tayari wapo wachezaji ambao tunawatazama na uongozi wa KVZ FC wapo nao katika mazungumzo," alisema.

Aidha, alisema wachezaji hao wapya watawatumia katika michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa majaribio na endapo watawaridhisha uongozi wa timu hiyo utaendelea na taratibu zote ili waichezee KVZ.

Alisema pia katika dirisha dogo timu hiyo itaachana na wachezaji wake sita ambao waliwasajili katika msimu huu, huku akieleza bado ni mapema kutaja majina yao kwa sasa.

Kocha huyo alisema sababu kubwa za kuachana na wachezaji hao ni kushuka kwa viwango vyao, majeruhi ya muda mrefu pamoja kutofanya vizuri katika mzunguko wa kwanza.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa KVZ FC kuendelea kutoa hamasa kwa timu hiyo hususan kuelekea katika michuano ya Kombe la Mapinduzi ambayo timu hiyo itashiriki.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS KUTUA JUVENTUS

KLABU ya Juventus inataka kumsajili kiungo wa kati Manchester City na England, Kalvin Phillips Januari, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 anaripotiwa kuwa tayari kuhama. ***(Tuttomercatoweb)***

### NKETIAH JANUARI PALACE

KLABU ya Crystal Palace imeonesha nia ya kumtaka mchezaji wa Arsenal na England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 24, wakati wa dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Transfers)***

### ARSENAL, CITY NA LUIZ

ARSENAL na Manchester City zote zinalenga kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, huku thamani yake ikitajwa kuwa ni pauni milioni 100. ***(Football Insider)***

### SANCHO MAMBO BADO

WAWAKILISHI wa winga wa England, Jadon Sancho, wanajaribu kulazimisha uhamisho wa kuondoka Manchester United, kwa nyota huyo, lakini makubaliano ya kubadilishana wachezaji kumhusisha winga huyo mwenye umri wa miaka 23, na Borussia Dortmund huenda yakawa magumu. ***(Givemesport)***

### ECHEVERRI ASAKWA CHELSEA

CHELSEA na Manchester City zimeomba kufahamishwa kuhusu kiungo wa kati wa River Plate raia wa Argentina, Claudio Echeverri, 17. ***(Fabrizio Romano)***

### ALABA ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kuwaondoa wachezaji msimu ujao ili kumsajili beki wa Real Madrid na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 31. ***(Fichajes)***

### NDIAYE ANUKIA EVERTON

EVERTON ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Marseille mwenye umri wa miaka 23 na raia wa Senegal, Iliman Ndiaye. ***(Teamtalk)***

### WIEFFER ALENGWA FULHAM

KLABU ya Fulham inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa Feyenoord na Uholanzi, Mats Wieffer, 24. ***(Football Insider)***

### GUTISERREZ ATAKIWA CITY

MANCHESTER City inatarajiwa kuungana na Real Madrid katika kinyang'anyiro cha kupata sahihi ya nyota wa Girona, Miguel Gutierrez, 22. ***(Manchester Evening News)***


### HOJBJERG KUTUA JUVE

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 28, yuko kwenye orodha ya Juventus ya uhamisho wa Januari. ***(Tuttosport)***

### PEAZ RASMI CHELSEA

KIUNGO wa Ecuador mwenye umri wa miaka 16, Kendry Paez atafanya mazoezi na Chelsea wiki ijayo. 'The Blues' walimsajili kutoka Independiente del Valle msimu uliopita kwa makubaliano ya kujiunga na klabu hiyo atakapotimiza umri wa miaka 18. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP ASHANGAA LIVER KUTOIFUNGA MAN UTD

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Liverpool waliitawala zaidi Manchester United katika suluhu ya Jumapili kuliko ushindi wa mabao 7-0 msimu uliopita dhidi ya timu hiyo ya Erik ten Hag, baada ya kuona kikosi chake kikikosa nafasi ya kuitoa Arsenal kileleni mwa Ligi Kuu England.

**Liverpool walipiga mikwaju 34 dhidi ya United waliokuwa na sita pekee, na walipata kona 12, huku kikosi cha Ten Hag kikimaliza dakika 90 bila kupata kona kwenye mchezo huo.**

Lakini licha ya ubabe wao, Liverpool hawakuweza kufunga na sasa watacheza na vinara wa ligi hiyo, Arsenal wakiwa na upungufu wa pointi moja kwenye Uwanja wa Anfield Jumamosi.

●●● Kama unacheza na timu yenye ubora kama United na wanalinda tu, basi haifanyi...

"Sikumbuki mchezo mkubwa kama huu dhidi ya Man United - hata tulipowafunga 7-0 hatukuwa hivi," alisema Klopp.

"Ulikuwa ni aina ya mchezo niloutarajia. Tukicheza hivi, ni vigumu kwa timu pinzani kutoka nje ya nusu yao na jinsi United walivyokuwa wakilinda ilikuwa safi kwao.

"Ukifunga, inabadilisha nguvu ya mchezo na wanafungua kidogo na kuchukua hatari zaidi. Lakini hakuna kilichobadilika, walitupa kila kitu.

"Kama unacheza Ligi Kuu na timu yenye ubora kama Man United na wanalinda tu, basi haifanyi maisha kuwa rahisi, tulipaswa kufunga na hiyo ingebadilisha mwelekeo wa mchezo."

Wakiwa wamepoteza 7-0 na 4-0 katika ziara zao mbili zilizopita pale Anfield, United walimaliza msururu wao mbaya wa matokeo ugenini kwa Liverpool licha ya kuwa bila wachezaji kadhaa muhimu kutokana na majeraha.

Na licha ya aina ya safu ya ulinzi ya kikosi chake, Ten Hag alisema ilikuwa ni hatua kubwa kwao.

"Kila nukta unayochukua ni muhimu," alisema Ten Hag.

"Kandanda inahusu matokeo, na tungeshinda leo (juzi) kama tungechukua nafasi zetu. Tunachukua hatua hii na tumefurahishwa na hatua hiyo kwa sababu Liverpool wako katika hali nzuri sana hapa Anfield".

# KANE HASHIKIKI BUNDESLIGA



**MUNICH,** Ujerumani

HARRY Kane amefikisha mabao 20 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wakati alipofunga bao moja katika kila kipindi na kuiongoza Bayern Munich kuibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya VfB Stuttgart Jumapili na kupunguza pengo la vinara Bayer Leverkusen hadi pointi nne wakiwa na mchezo mkononi.

Nahodha huyo wa England aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 100 kutoka Tottenham Hotspur msimu huu, amefunga mara 20 katika mechi zake 14 za ligi hadi sasa.

Yeye ni mchezaji wa tatu tu katika historia ya ligi hiyo kufikisha mabao hayo kabla ya hatua nusu ya msimu, akiwa sambamba na Robert Lewandowski na Gerd Muller.

Licha ya kuandamwa na majeraha na kukosekana dakika za mwisho kutokana kuugua kwa Joshua Kimmich Leon Goretzka, Bayern walifikisha pointi 35 wakiwa na mchezo mmoja mkononi, huku Leverkusen wakiwa kileleni na pointi 39.

"Pengine ilikuwa uchezaji wetu bora zaidi wa msimu hadi sasa," alisema Kane.

"Tulitaka kuwatawala. Tulijua jinsi walivyokuwa hatari na tulipunguza kwa nafasi chache tu. Ilikuwa nzuri kufunga mara mbili na kuisaidia timu."

Ligi hiyo inachukua mapumziko baada ya mechi za wiki ijayo na itaendelea Januari 12.

Bayern walikuwa na nia ya kurejea kutoka kipigo cha mabao 5-1 wiki iliyopita dhidi ya Frankfurt na walihitaji dakika mbili tu kufunga.

# Madrid kusajili beki Januari



**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema "sijawahi kuona majeruhi watatu kwa muda wa miezi minne" baada ya David Alaba kujiunga na Thibaut Courtois na Eder Militao kwenye orodha ya majeruhi wa muda mrefu wa Real Madrid, huku kocha huyo akisema klabu hiyo sasa inaweza kufikiria kununua beki Januari.

Beki wa kati Alaba alitolewa katika dakika ya 35 ya ushindi wa 4-1 wa Madrid wa LaLiga dhidi ya Villarreal Jumapili baada ya kuumia goti lake la kushoto alipokuwa akigombea mpira katika Uwanja wa Santiago Bernabeu.

"Baada ya kufanyiwa vipimo, mchezaji wetu David Alaba aligundulika kuwa na mpasuko wa mishipa kwenye goti lake la kushoto," ilieleza taarifa ya Madrid.

"Sijazungumza na Alaba," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ni aibu, kwa hakika. Tuna huzuni kubwa kumpoteza mchezaji mwingine. Sijawahi kuona majeruhi watatu muda wa miezi minne. Ni ajabu. Lakini hakuna tunachoweza kufanya.

"Kinachotakiwa kukifanya kwa timu ni kile ambacho imefanya kwa majeruhi wote tuliowapata, ambapo ni kukaa kimya, tumefanya zaidi ya watu walivyofikiria, pamoja na matatizo yetu yote, timu hii inapambana na dhamira ya ajabu.

"Ndiyo njia pekee tunaweza kuchukua nafasi ya wachezaji wote muhimu ambao wamepata majeraha. Tutaona katika siku chache zijazo kama tunaweza kufanya kitu."

Ferland Mendy pia alitolewa wakati wa mapumziko kwa tatizo la misuli, huku Dani Carvajal, Eduardo Camavinga, Arda Guler na Vinicius Junior wakiwa nje ya uwanja na Militao na Courtois.

"Nadhani atafanya mazoezi na timu Jumanne," alisema Ancelotti kuhusu Carvajal.

# Arteta afichua siri ya kiwango cha Havertz

**LONDON,** Emgland

MIKEL Arteta amesisitiza kwamba 'kujiamini' kwa Kai Havertz kumekuwa ufunguo wa kuboresha kiwango chake kwa Arsenal katika wiki za hivi karibuni.

'Washikabunduki' hao walitoa kitita cha pauni milioni 65 ili kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani kutoka Chelsea wakati wa usajili wa majira ya joto, lakini Havertz alitatizika sana katika miezi yake ya kwanza hapo Kaskazini mwa London.

Kutokana na mwanzo huo mgumu wa maisha ndani ya Arsenal, Havertz anaonekana kurejea kwenye kiwango chake - akifunga mabao manne hadi sasa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ubora wa Havertz baada ya Mjerumani huyo kufunga bao lingine katika ushindi muhimu dhidi ya Brighton and Hove Albion Jumapili, kocha Arteta alisisitiza kwamba kujiamini kumekuwa ufunguo wa kuimarika kwa mchezaji huyo.

"Kujiamini kwake kunaongezeka na anajiona yuko salama zaidi uwanjani, kitendo cha kufunga bao moja kilisaidia kufunga la pili, ni mechi nne kati ya saba sasa," alisema. Arteta.

"Lakini kwa ujumla, uchezaji wake, akili anayoonesha uwanjani na jinsi anavyofanya kazi kwa kujilinda, ni ya hali ya juu na ni nzuri sana."

Akizungumzia ushindi wenyewe, Arteta aliwasifu wachezaji wake akisema: "Pongezi kubwa kwa timu na kwa wachezaji. Nadhani tulikuwa na kiwango cha kuvutia.

"Nadhani tulistahili kushinda mchezo huo. Lazima niwasifu kwa sababu najua jinsi ugumu ulivyo na kile Brighton walifanya kama timu. Hatukuruhusu hilo kutokea, kwa hivyo nina furaha kubwa."



# Wachezaji Yanga sasa wampa kiburi Gamondi

INATOKA UKURASA 24

wa mechi.

"Kutunza nguvu za wachezaji ni jambo jema, angalia tulisafiri sana, tumecheza mechi nyingi zilizokaribiana na mwezi huu tuna mechi nyingi zaidi na wachezaji ni hawa hawa, kwa hiyo niliona ni heri kuwapa nafasi baadhi ya wachezaji ili wengine wapumzike kwa mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema.

Kocha huyo raia wa Argentina alifurahi kuona wachezaji wengi walioanza ambao awali hawakuwa wanaanza na wale aliowafanyia mabadiliko wameonesha viwango vya hali ya juu katika mechi dhidi ya Mtibwa ambayo Yanga ilitoka na ushindi wa mabao 4-1.

"Wameonesha viwango vizuri, lakini kubwa ambalo linanifurahisha ni kupumzika kwa baadhi ya wachezaji tegemeo, najua kuna wengine wana adhabu na wengine wawili ni majeruhi, lakini wengine niliwapumzisha ili warudishe nguvu zao kwa ajili ya mechi inayofuata," alisema.

Wachezaji ambao hawakucheza kabisa mechi ya Jumamosi ni Joyce Lomaliza, Yao Kouassi, Dickson Job, Khalid Aucho ambaye ana adhabu ya kufungiwa, huku Pacome Zouzoua akiingia kipindi cha pili.

Kocha huyo aliwapa nafasi ya kuanza wachezaji ambao hawajaonekana kwa kipindi kirefu, kama vile Mahlatse Makudubela 'Skudu', Cripin Ngushi aliyeingia kuchukua nafasi ya Jesus Moloko, Gift Fred aliyechukua nafasi ya Bakari Mwamnyeto na Farid Mussa akitwaa nafasi ya Maxi Nzengeli, wakati Nickson Kibabage nafasi yake aliingia Pacome baadaye.

Kesho Yanga itacheza mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu dhidi ya Medeama kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambapo inahitaji ushindi kwa udi na uvumba ili kurudisha matumaini ya kusonga mbele kwenye hatua ya robo fainali.

Ikiwa ugenini, Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya timu hiyo, Desemba 8, mwaka huu na kuwa sare ya pili kwenye michuano hiyo ikiwa Kundi D, huku ikiwa imepoteza mchezo mmoja.

Inashika nafasi ya mwisho ikiwa na pointi mbili baada ya kucheza mechi tatu na kama itashinda itafikisha pointi tano ambazo kwa sasa inazo Al Ahly inayokamata usukani, huku yenyewe haitokuwa dimbani kucheza dhidi ya CR Belouizdad baada ya mechi hiyo kuahirishwa kutokana na ushiriki wa Wamisri hao kwenye michuano ya Klabu Bingwa Dunia inayoendelea nchini Saudi Arabia.

# KLABU Z'BAR ZATAKA KANUNI POINTI ZA MEZANI KUFUTWA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Mashindano ya Chama cha Soka Mkoa wa Mjini Magharibi (UWERFA), imekutana na Makatibu wa Klabu za Ligi ya Mkoa huo pamoja na makocha wao kwa ajili ya kufanya tathmini ya mzunguko wa kwanza wa Ligi ya Mkoa, uliomalizika Jumamosi iliyopita.

**Katika kikao hicho viongozi wa klabu kilichofanyika mkoani humo jana, walitoa mapendekezo yao hasa katika masuala ya kanuni kuhusu vifungu ambavyo katika mzunguko huu vilitumika kutoa alama tatu za mezani.**

Walitaja vifungu hivyo kuwa ni pamoja na sura ya 15 ambayo timu itakayochelewa kwa saa sita kabla ya mchezo kujaza 'listi' ya wachezaji itakayowatumia katika mchezo husika itakuwa imepoteza mchezo huo.

Kingine ni sura ya 29, ambayo inaeleza mchezaji wa timu itakayempiga mwamuzi timu hiyo itapokonywa alama tatu katika mchezo huo na alama tatu nyingine zitatolewa katika msimamo wa ligi hiyo.

Pia sura ya 16 timu mwenyeji iwapo itashindwa kulipa pesa ya waamuzi wa mchezo katika kikao cha matayarisho ya mechi au kutokwenda katika kikao hicho, itakuwa imepoteza mchezo na timu pinzani itapewa alama tatu.

Kifungu kingine ni sura ya 17 ambayo kiwanja ambacho hakitokuwa na alama za uwanjani na mwamuzi akithibitisha hilo, timu hiyo itakuwa imepoteza mchezo huo.

Akizungumza katika kikao hicho, Katibu wa timu ya Urafiki FC, Suleiman Mzee, alisema katika kipindi hiki cha mapumziko ya dirisha dogo Chama cha Soka Mkoa Kifanye mapitio ya kanuni hizo ili kuweza kufanya marekebisho madogo ambayo yatasaidia mzunguko wa lala salama klabu kutopata alama za mezani kama ilivyokuwa mzunguko wa kwanza.

Alishauri lazima kuwapo na kanuni rafiki ambazo zinaendana na Ligi ya Mkoa hasa katika viwanja ambavyo vinatumika kwa ligi hiyo mara nyingi hujaa maji pale mvua kubwa inaponyesha na kusababisha alama zilizochorwa kufutika.

Alisema asilimia kubwa katika timu 23 zinazocheza ligi hiyo, nyingi zinatumia viwanja vyenye nyasi asilia na alama zake huwekwa kwa chokaa au mchanga wa baharini, hivyo changamoto ya mvua kubwa husababisha kufutika.

"Kanuni yetu inazibana sana klabu zetu hasa timu mwenyeji. Kanuni inaongoza kutoa alama tatu za mezani, hii si nzuri katika soka, yaani timu mwenyeji uwanja wako kama alama hazionekani umepoteza mchezo, hujaenda katika kikao cha matayarisho ya mechi umepoteza mchezo, kadhalika kama hujatoa pesa ya waamuzi ni hivyo hivyo, sasa bora tuweke adhabu ya faini badala ya kupoteza mchezo kwa kupewa alama tatu mpinzani wako," alisema.

Katibu wa Chama cha Soka Mkoa huo, Maalim Ahmada, alizitaka klabu kuhakikisha zinapeleka mtu sahihi na mwenye maamuzi katika klabu pale wanapofanya marekebisho ya kanuni kwa kila msimu unapofika.

Alisema kanuni inayotumiwa msimu huu imetokana na maoni ya viongozi wa klabu waliyopendekeza na kuyapitisha kwa pamoja ndipo kabla ya kuanza kutumika.

"Changamoto iliyopo ni klabu nyingi inaonekana bado hamna uongozi uliokamilika hili ndilo linaleta huu mgogoro au changamoto mnayoiona, maana kanuni hii inatokana na maoni yenu ambayo tulikutana na kufanya maamuzi ya pomoja, sasa hili la kuoneana kuwa kanuni inabana sijui limetoka wapi wakati tumelipitisha kwa pamoja," alisema.

Hata hivyo, alisema maoni yote yaliyotolewa na viongozi hao wa klabu yatawasilishwa kwa Kamati ya Utendaji ya UWERFA ili kuona namna gani yatafanyiwa kazi kabla ya kuanza kwa mzunguko wa lala salama.

## AAAH WAPI!...



Kipa wa Machester United, Andre Onana, akiinusuru timu yake kufungwa dhidi ya Liverpool katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Anfield na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

# *Benchikha: Njooni muone hii ni fainali*

INATOKA UKURASA 24

Nahodha Msaidizi wa Simba, Tshabalala, alisema wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo ili waweze kujiweka katika mazingira mazuri.

"Huu ni mchezo muhimu kwetu kupata matokeo, tunasahau yaliyopita na kuanza upya wachezaji wako vizuri tunaamini tutaenda kufanya vizuri kwenye mchezo huu," alisema.

Kocha Mkuu wa Wydad Casablanca, Mtunisia Faouzi Benzarti, ambaye huo utakuwa mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa kuiongoza timu hiyo baada ya kutwaa mikoba ya Adil Ramzi, aliyetimuliwa wiki iliyopita, alisema mchezo huo utakuwa mgumu ila wamejiandaa kutafuta ushindi.

Alisema wanaifahamu Simba vizuri na mechi ya mwisho katika uwanja huu walipoteza ila wamekuja kivingine kuhakikisha wanashinda na kupata pointi.

"Tutaiheshimu Simba kulingana na ubora wao na ukizingatia mechi ya kwanza ilionesha kiwango kuzuri na kuleta ushindani na kuweza kupata ushindi dakika za mwisho," alisema Benzarti.

Naye mwakilishi wa wachezaji wa Wydad Casablanca, Moutie Yousse, alisema wanatambua ubora wa Simba kikubwa wanaenda kufuata kile ambacho walipewa katika uwanja wa mazoezi.

"Tumejiandaa vizuri, tutacheza kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunafanikiwa katika malengo yetu ya kupata ushindi kwenye mchezo wetu wa pili licha ya kwamba utakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa Simba," alisema Yousse.

Michezo
Jumanne Desemba 19, 2023
Nipashe



Klopp ashangaa Liver kutoifunga United UKURASA 21

UEFA CHAMPIONS LEAGUE

**HATUA 16 BORA UEFA**

| | | |
|---|---|---|
| Porto | vs | Arsenal |
| Napoli | vs | Barcelona |
| PSG | vs | Real Sociedad |
| Inter | vs | Atletico Madrid |
| PSV | vs | Borussia Dortmund |
| Lazio | vs | Bayern Munich |
| Copenhagen | vs | Ma City |
| RB Leipzig | vs | Real Madrid |



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad ya Morocco itakayopigwa uwanjani hapo leo saa 10:00 alasiri. **PICHA: SIMBA**

# Benchikha: Njooni muone hii ni fainali

## ●●● Wachezaji wapania kupambana kiume leo, Wydad wenyewe wasema...

**Na Saada Akida**

WAKATI leo wakishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Wydad Casablanca ya Morocco kwenye mchezo wa marudiano wa Kundi B Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha na nahodha msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala', wamewaita mashabiki uwanjani hapo huku wakisema "hii ni kama fainali kwetu".

**Simba leo wanashuka dimbani hapo kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo utakaopigwa saa 10:00 alasiri huku wakiwa na kumbukumbu ya kuichapa Wydad bao 1-0 katika uwanja huo kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo msimu uliopita shukrani zikimwendea Jean Baleke aliyeizamisha.**

Lakini pia kwa Simba, huo utakuwa mchezo wakutaka kulipa kisasi cha kufungwa bao 1-0 msimu uliopita katika mechi ya marudiano ya robo fainali nchini Morocco na kipigo kama hicho msimu huu zilipokutana nchini humo kwenye mechi ya Kundi D.

Huu unakuwa mchezo wa pili kuzikutanisha timu hizi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo mara ya mwisho Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na Jean Baleke.

Hata hivyo, Simba inashuka uwanjani kwenye mchezo huu ikiwa mkiani mwa Kundi B na alama mbili baada ya mechi tatu kupoteza moja na sare mbili. Kundi hilo likiongozwa na Asec Mimosas ya Ivory Coast yenye pointi saba iliyotoka nayo sare ya bao 1-1 na kisha Simba kwenda kupata suluhu ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana inayoshika nafasi ya pili ikiwa na ponti nne moja mbele ya Wydad.

Kuelekea mechi hyo Kocha Mkuu wa Simba, Benchikha, ameliambia Nipashe jana, haitakuwa rahisi na kwamba ni fainali yao, hivyo wamejipanga kuhakikisha wanashinda ili kuwafurahisha mashabiki wao na kutimiza malengo yao.

Alisema ni mechi muhimu kwao kupata matokeo, hivyo wanapaswa kuwa imara ili kushinda na kurejesha matumaini yao ya kusonga hatua inayofuata.

"Wydad ni timu kubwa, tumecheza nao Marrakesh na kuonesha mchezo mzuri, ninaimani na wachezaji wangu wataenda kujitoa ili tupate ushindi na kuwafurahisha mashabiki wetu.

"Naenda kukutana na Wydad yenye kocha mpya ambaye ni kocha mkubwa na mzoefu, lakini rafiki yangu, namjua vizuri haitakuwa rahisi malengo yetu ni kushinda mchezo huu," alisema Benchikha.

Alisema anawaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kuwapa sapoti ili waweze kupata ushindi katika mchezo huo ambao umebeba matumaini yao kwenye hatua ya makundi.

INAENDELEA UKURASA 23



Mudathir Yahya akiwa mazoezini Yanga.

# Wachezaji Yanga sasa wampa kiburi Gamondi

**Na Adam Fungamwango**

KUPUMZIKA kwa baadhi ya wachezaji na wengine kupata dakika chache za kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar Jumamosi iliyopita, kumempa kiburi Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, kufanya vema katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kesho, Jumatano dhidi ya Medeama ya Ghana.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Gamondi alisema alikuwa akiumiza kichwa ni jinsi gani anaweza kutunza nguvu za wachezaji wake kuelekea kwenye mechi hiyo kwani ratiba inaonesha kuwa kutakuwa na mechi nyingi za Ligi Kuu na Kombe la FA, lakini sasa ana uhakika kwenye mechi hiyo atakuwa na baadhi ya wachezaji ambao hawana uchovu

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042